# KUCHUNGUZA TAMATHALI ZA SEMI KATIKA KUIBUA DHAMIRA KATIKA RIWAYA YA MBALI NA NYUMBANI

**ISSA KHAMIS MBAROUK**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUPATIA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI FASIHI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

# UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma kazi hii na anaidhinisha ikubaliwe kwa utahini na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tasnifu hii inayoitwa: ***"Kuchunguza Tamathali za Semi katika Kuibua Dhamira katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani"*** na kupendekeza ikubaliwe kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Shahada ya (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

………………………..……......

Prof. Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

…………………………………

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairusiwi kuiga au kumiliki kwa namna yoyote ile sehemu ya tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

# IKIRARI

Mimi, **Issa Khamis Mbarouk**, ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

……………………………………..

Saini

……………………………………..

Tarehe

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu, Bwana Khamis Mbarouk na Bibi Mayasa Hamad kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, kunifunza mema, kunikataza mabaya, na kunipa moyo na kuniwezesha kifikra na maadili mema katika kipindi chote cha masomo yangu, tangu darasa la kwanza mpaka sasa ninapokamilisha masomo yangu ya shahada ya Uzamili. Mawazo yao na busara zao katika elimu nitazikumbuka daima na kuwa chachu ya kujiendeleza zaidi.

Vile vile ninamtabarukia mke wangu kipenzi Rehema Juma, kwa ushawishi, uvumilivu, huruma na kunitia moyo pale nilipokata tamaa katika masomo yangu. Pia kwa msaada wa hali na mali katika kukamilisha masomo yangu, ikiwa ni pamoja na gharama za masomo na kuwa msimamizi na nguzo imara na thabiti katika kukamilisha sikati tamaa ila ninamaliza masomo yangu. Pia ninawatabarukia wanangu Khamis Issa, Zeyana Issa, Yusra Issa na Anuari Issa, kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha masomo yangu. Nimatumaini yangu kuwa wataweza kutambua umuhimu wa Elimu katika maisha ya mwanadamu ili iwe ni changamoto kwao.

Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitomshukuru mwajiri wangu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA), kwa mchango wake mkubwa iliyonipatia ikiwa ni pamoja na kuniruhusu kujiunga na masomo haya na kunipa ruhusa ya kufuatilia masomo yangu pale nilipohitaji.

## SHUKURANI

Kwanza, napenda kumshukuru mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi muweza wa kila kitu, kwa kunijaalia afya njema, nguvu, uwezo, akili, busara, maarifa, utulivu na uvumilivu katika kipindi chote cha masomo yangu ya Uzamili.

Pili, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa, Msimamizi wangu Prof. Emmanuel Mbogo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala hakuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Amenilea kitaaluma na kunipa moyo pamoja na kunifunza misingi ya nadharia ya fasihi na mbinu za utafiti ambazo zimezaa kazi hii. Namuomba Mwenyezi Mungu ambariki na ampe afya njema pamoja na ukakamavu na amzidishie kila la kheri, na kumuepushia kila la shari.

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu uchunguzi wa tamathali za semi katika kuibua dhamira katika riwaya ya Shafi Adam Shafi. *Mbali na Nyumbani*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya tamathali za semi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* (2013) ya Shafi Adam Shafi, ili kuona jinsi gani tamathali zimetumika kisanii katika kuibua dhamira katika kazi hii. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum, wakati ambapo data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya mapitio ya maandishi. Data zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui. Uchunguzi, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti huu yaliongozwa na nadharia ya Simiotiki. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa, Shafi Adam Shafi ametumia tamathali za semi kama mbinu ya kimtindo katika kuibua dhamira za kazi yake. Hii ni kusema kwamba Shafi Adam Shafi anaendelea kuitumia mbinu ya tamathali za usemi kama kibainishi chake cha mtindo katika kazi zake za riwaya. Riwaya ya *Mbali na Nyumbani* imeathiriwa zaidi na matumizi ya tashibiha ikifuatiwa na tashihisi na tamathali nyengine zimetumika katika kuongeza nguvu ya ufahamu wa riwaya hiyo.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO ................................................................................................ ii**

**HAKIMILIKI ................................................................................................ iii**

**IKIRARI ................................................................................................ iv**

**TABARUKU ................................................................................................ v**

**SHUKURANI................................................................................................ vi**

**IKISIRI ................................................................................................ vii**

**YALIYOMO ................................................................................................ viii**

**ORODHA YA MAJEDWELI ................................................................ xii**

**SURA YA KWANZA................................................................................ 1**

1.1 Usuli wa Mada ................................................................................ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ................................................................................ 7

1.3 Lengo la Utafiti ................................................................................ 8

1.3.1 Malengo Mahsusi ................................................................................ 8

1.4 Mwaswali ya Utafiti ................................................................................ 8

1.5 Umuhimu wa Utafiti................................................................................ 9

1.6 Mipaka ya Utafiti................................................................................ 9

1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake.................................................. 10

1.8 Mpangilio wa Tasnifu................................................................................ 11

1.9 Hitimisho ................................................................................ 11

**SURA YA PILI ................................................................................ 12**

**MAPITO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA............. 12**

2.1 Utangulizi................................................................................ 12

2.2 Ufafanuzi wa Istilahi ................................................................... 12
2.2.1 Maana ya Riwaya ........................................................................ 12
2.3 Chimbuko la Riwaya ................................................................... 13
2.4 Maana ya Tamathali za Semi ................................................................ 17
2.5 Tafiti Kuhusu Riwaya za Shafi Adam Shafi .............................................. 18
2.5.1 Tafiti Kuhusu Tamathali za Semi.......................................................... 24
2.6 Kiunzi cha Nadharia ................................................................... 26
2.6.1 Nadharia ya Simiotiki ................................................................. 27
2.6.2 Sababu ya Kuchagua Nadharia ya Simiotiki.......................................... 31
2.6.3 Nadharia ya Simiotiki ilivyotumika ......................................................... 32
2.6.4 Kufaa kwa Nadharia Iliyotumika ............................................................... 32
2.7 Hitimisho ........................................................................................ 33
**SURA YA TATU.................................................................................... 34**
**MBINU ZA UTAFITI............................................................................. 34**
3.1 Utangulizi.......................................................................................... 34
3.2 Eneo la Utafiti ..................................................................................... 34
3.3 Usanifu wa Utafiti ................................................................................ 35
3.3.1 Umuhimu wa Usanifu wa Utafiti ............................................................ 35
3.4 Kundi Lengwa ........................................................................................ 36
3.5 Sampuli na Usampulishaji ........................................................................ 37
3.6 Aina ya Data ........................................................................................ 38
3.6.1 Data za Msingi ..................................................................................... 38
3.6.2 Data za Upili ........................................................................................ 38
3.7 Mbinu za Kukusanya Data ........................................................................ 39

3.7.1 Mbinu ya Usomaji Machapisho ................................................................ 40

3.7.2 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu.............................................................. 41

3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data ............................................................... 41

3.9 Hitimisho .................................................................................................. 42

**SURA YA NNE ........................................................................................... 44**

**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.......................................... 44**

4.1 Utangulizi................................................................................................... 44

4.2 Muhtasari wa Riwaya Teule.................................................................... 45

4.2.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ...................................... 45

4.2.2 Maudhui katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani ........................................ 46

4.3 Wasifu wa Mwandishi ................................................................................ 46

4.4 Usimulizi katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani ...................................... 47

4.4.1 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza.............................................................. 48

4.4.2 Matumizi ya Nafsi ya kwanza wingi ..................................................... 48

4.5 Ubainishaji wa Tamathali za Usemi katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani ................................................................................. 49

4.6 Ubainishaji wa dhamira katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani........... 52

4.6.1 Tashibiha.................................................................................................... 52

4.6.1.1 Tashibiha na Uibuaji wa Dhamira katika *Mbali na Nyumbani*............. 53

4.6.2 Tashihisi..................................................................................................... 55

4.6.3 Takriri ....................................................................................................... 58

4.6.4 Methali ...................................................................................................... 60

4.6.5 Tanakali Sauti............................................................................................ 63

4.7 Hitimisho ................................................................................................... 65

**SURA YA TANO ... 67**

**MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... 67**

**5.1 Utangulizi ... 67**

**5.2 Muhutasari ... 67**

**5.3 Hitimisho ... 71**

**5.4 Mapendekezo ... 71**

**MAREJELEO ... 73**

## ORODHA YA MAJEDWELI

Jedweli Na. 4.1: Tamathali za Usemi .................................................................... 51

Jedweli Na. 4.2: Tashibiha na Uibuaji wa Dhamira katika Mbali na Nyumbani ............................................................................ 53

Jedweli Na. 4.3: Tashihisi na Uibuaji wa Dhamira katika Riwaya ya *Mbali na Nyumbani*............................................................ 56

Jedweli Na. 4.4: Takriri na Uibuaji wa Dhamira katika Riwaya ya *Mbali na Nyumbani* .................................................................. 59

Jedweli Na. 4.5: Methali na uibuaji wa Dhamira katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani .................................................................. 62

Jedweli Na. 4.6: Tanakaulisauti na Uibuaji Dhamira katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani............................................................ 64

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Wataalamu mbali mbali wameeleza na kufafanua maana ya riwaya. Kutokana na ufafanuzi huo ni dhahiri kuwa kuna maoni mbali mbali yanayohusu dhana ya riwaya. Wataalamu wote wamekiri kuwa riwaya ni utanzu wa fasihi andishi, ikiwa ni pamoja na ushairi na tamthiliya. Matteru (1976) anafafanua kuwa riwaya ni hadithi ndefu ambazo zimeandikwa. Kutokana na maana hii tunaweza kuona mambo matatu makuu katika dhana ya riwaya, kwamba riwaya ni hadithi, hadithi ni lazima iwe ndefu na ni lazima iwe imeandikwa.

Kwa mujibu wa Abbas; Mphalale (1976, anasema riwaya ni hadithi ndefu za maneno kati ya 35,000 na 50,000.Tunaweza kusema kwamba kuna riwaya ndefu na riwaya fupi, kulingana na idadi ya maneno yaliyotumiwa na mwandishi. Mulokozi (1996) anaeleza kuwa, riwaya ni kazi ambayo inakuwa na sifa mbali mbali, kuwepo na ubunifu, usimulizi (ni hadithi ya kisimulizi la kinadhari), mpangilio au msukumo fulani wa matukio (ploti), mfungamano wa wakati, visa vinatendeka katika wakati fulani, inatakiwa iwe na maneno mengi na itakapokuwa na maneno pungufu ya elfu tatu (3,000), yaweza kuitwa Novela, pawepo na mawanda mapana (kwa upande wa yale yanayozungumzwa, wakati na mahali pa matukio hayo), na pia pawepo na uchangamani katika visa, dhamira, tabia, wahusika n.k. Senkoro (1982) na Wamitila (2002) wanaeleza kuwa riwaya ni kisa mchangamano ambacho chaweza kuchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kifani na kimaudhui. Kisa

ambacho urefu unaoruhusa kisa kitambe na kutambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwanadamu.

Hivyo riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana maisha ya jamii. Kuhusiana na chimbuko au chanzo cha utanzu huu wa fasihi, wataalamu wengi au wote wanakubaliana na chanzo cha riwaya ni hali halisi ya jamii, pia wanakubaliana kuwa utanzu huu ni mchanga, ukilinganisha na tanzu kama ushairi, michezo ya kuigiza au tamthiliya.

Ndungo na mwenzake (1991) wanasema kuwa, miongoni mwa riwaya za mwanzo kuzuka ilikuwa ni riwaya ya Robinson Cruisoe (1719) ya Daniel Defoe. Riwaya hii ilizuka kutokana na maendeleo na mabadiliko ya uvumbuzi wa viwanda. Ukoloni wa uvumbuzi wa viwanda ulileta haya ya kueleza mambo kwa njia ya hadithi na ngano ambazo zilikuwepo kwa wakati huo. Wanaendelea kusisitiza kuwa, kuzuka kwa miji na viwanda kulistawisha uandikaji wa riwaya na usomaji kupanuka. Maendeleo katika vipengele vyote vya maisha kama vile kiuchumi, kisiasa na kijamii, yalizusha haja ya kuwa na utanzu wa fasihi ambao uchangamano wake wa kifani na kimaudhui ungedhibiti nyanja hizi zote.

Akijadili kuhusu kuzuka kwa riwaya Mulokozi (1996) anasema kuwa riwaya haikuzuka hivi hivi tu, bali ilitokana na fani za masimulizi (za hadithi) zilizokuwepo kabla. Hivyo fani hizo zilikuwemo katika fasihi simulizi iliyokuwepo kabla ya kuzuka utanzu wa riwaya katika fasihi andishi, na

ziliigizwa na watunzi wa mwanzo wa riwaya. Watunzi hao walisukumwa na mabadiliko ya kijamii ya karne ya 16 -18 huko Ulaya. Fani ya jadi ambazo zilichangia katika kuchapuza riwaya ni ngano, hekaya, tendi, visakale, historia, siasa, masimulizi ya wasafiri, insha na tafsiri.

Hoja za Ndungo na wenzake (1991) pamoja na Mulokozi (1996) zinadhihirisha kuwa, riwaya ilianzia huko Ulaya, kutokana na mabadiliko mbali mbali ya kijamii yaliyotokea nchi za Ulaya na kuathiri wanajamii. Masimulizi yaliyokuwepo kabla ya mabadiliko hayo ndiyo yaliyotumika kuweza kuonya, kuburudisha, kuliwaza, kutunza historia ya jamii, kwa kutumia mfumo wa maandishi ambapo yalikuwa ni maendeleo mapya katika dunia. Hali hii inayothibitisha kuwa fasihi lazima kuendana na mabadiliko ya jamii.

Mulokozi (1996) anasisitiza kuwa kufika karne ya kumi na sita (16), fani zilizotajwa kama vile ngano, hekaya, tendi, visakale, historia, insha na tafsiri, zilikuwa zimeshaenea pia kufahamika na mataifa mengi. Hivyo kulihitaji msukumo wa jamii kiteknolojia na kiuchumi ili ziweze kuwa riwaya.

Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa, palikuwepo na mambo yaliyopelekea kuenea kwa vitu hivyo ndani ya jamii. Hivyo ilipelekea ukuaji mkubwa wa shughuli za kiuchumi huko Ulaya. Ukuaji huo ulishikamana na biashara za masafa marefu za baharini kutoka bara moja hadi bara jengine. Vile vile msukumo mwengine ni kuvumbuliwa kwa Mabara ya Afrika pamoja na kukua kwa vitendea kazi (nyenzo) vya uzalishaji wa viwandani barani Ulaya. Hali iliyosababisha mapinduzi ya iwanda. Chanzo cha riwaya katika fasihi ya Kiswahili

ni fani za kijadi ni ngano, hekaya, tendi, visakale, historia, sira, masimulizi ya wasafiri, insha na tafsiri. Watoto na wazee walikuwa wanakutana na kutambiana hadithi kwa njia ya kushauri, kuonya, kutahadharishana na kuelezana mambo mbali mbali kuhusu jamii. Hadithi hizi zilipokezwana kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Wataalamu hawa wanakubaliana kuwa ujio wa Wazungu karna majilio ya wageni waliotangulia katika Afrika ya Mashariki, yalikuwa na athari kubwa katika fasihi ya Kiswahili. Kwani hati za Kilatini zilianza kutumika mwaka 1890 kwa watu wa Afrika Mashariki, na yale yaliyoandikwa na walimu wenyewe kwa kutumia mila na tamaduni za kwao. Kulikuwa hakuna yaliyoandikwa na Waafrika kwa wakati huo. Hivyo hadithi za Waafrika zilikuwa katika masimulizi.

Maelezo hayo yanathibitisha kuwa riwaya ni mawazo ya Afrika na mawazo ya wageni wa kizungu. Mara nyingi vitabu hivi vilijikita kuelezea tajriba yao ya maisha, silka malezi na mtazamo kuhusu maisha. Pia waliendelea kutunga vitabu vya hadithi vya Kiarabu na Kizungu, baadhi ya vitabu hivyo ni kama vile Alfulela Ulela (1313), Safari ya Gulliver (1932), Mashimo ya Mfalme Suleiman (1929), Hekaya za Abunuasi (1915) n.k.

Waafrika walitunga hadithi kwa kutumia maudhui na mtindo katika mtiririko wa visa na mengineyo yaliyoegemea katika kuendeleza ukoloni na utamaduni wa kigeni. Riwaya ziliendelea kutungwa kwa kuziba pengo la ukosefu wa riwaya katika fasihi ya Kiswahili. Palianzishwa mashindano ya uandishi na taasisi ya kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa utungaji wa hadithi fupi pamoja na vitabu vidogo vidogo na lugha iliyotumiwa ni ile iliyokubaliwa na taasisi

hiyo, na mfano wa vitabu ni Mjomba Remus (1935), Safari ya Juma (1949), Safari ya Sungura (1926) n.k.

Hadithi na vitabu vilivyotungwa havikusaidia ila kukuza nadharia za kuendeleza na kudumisha Ukoloni na kudunisha utamaduni wa Kiafrika, ijapokuwa havikusaidia kwa kiasi fulani lakini hali hii ilipelekea kuibua waandishi wa riwaya za Kiswahili.

Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa chanzo cha riwaya za Kiswahili, ni mchango mkubwa uliotokana na biashara na Mapinduzi ya viwanda huko Ulaya. Hali hii ilianza Ulaya na kuja Afrika kwa kutumia biashara ya baharini. Ambapo biashara hii ilipotokea Ulaya kuja Afrika iliathiri kwa kiasi kikubwa mila, silka za desturi za Waafrika.

Hali iliyopelekea kufuta uhalisia wa Kiafrika na kuwa mchanganyiko kati ya Uafrika na Uzungu. Ndipo palipopatikana kitu kiitwacho riwaya inayotokana na fasihi andishi baada ya hadithi inayotokana na fasihi simulizi. Hata hivyo tukirejelea mawazo ya Mulokozi (1996), yanaonesha kuwa riwaya ya Kiswahili imechimbuka katika fasihi simulizi.

Riwaya kama ilivyo kazi zingine za fasihi hutumia lugha ya kisanii ili kuipa ujumi wa kifasihi. Fasihi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kuwakilisha ujumbe kwa hadhira kwa njia ya maandishi ama mdomo na vitendo (Mulokozi 1996). Katika uandishi wa riwaya, waandishi wa kazi za fasihi hutumia lugha inayolingana na mandhari na mazingira ya jamii husika ili kujenga na

kupelekea kuibuka kwa ujumbe au maudhui ya kazi hiyo. Kwa hivyo utumiaji wa lugha kisanaa ndio kiini cha kuibuka kwa ujumbe uliomo katika riwaya husika na katika kazi yoyote ile ya fasihi. Utafiti wetu unahusu uchunguzi wa tamathali za usemi ambacho ni kipengele kimoja wapo cha lugha kinachotumiwa na wasanii katika uibuaji wa dhamira walizozikusudia.

Hivyo basi mtafiti wa utafiti huu alikusudia kuchunguza tamathali za semi ambacho ni kipengele cha fani ili kubaini kwa namna gani kinaweza kuibua dhamira za msanii. Katika utafiti wetu, tulichunguza tamathali za semi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi na kuona ni jinsi gani tamathali za semi zinatumika katika kuibua dhamira zilizomo katika riwaya hiyo. Kwa kufanya hivi tumeweza kuonesha uhusiano wa fani na maudhui kama ambavyo umekuwa ukishadidiwa na wataalamu mbali mbali kuwa ni dhana ambazo haziwezi kutenganishwa na zinategemeana.

Swali letu la msingi ni kuona ni jinsi gani Shafi Adam Shafi anatumia lugha ya kitamathali kisanii katika kuwasilisha dhamira za kazi zake. Katika kutafiti tafiti mbali mbali tumebaini kuwa tafiti nyingi hazikulenga kuchunguza tamathali za semi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*,hali ambayo imetutia hamasa ya kufanya utafiti huu unaohusu tamathali za semi ili kuweza kubaini kwa namna gani tamathali za semi zinaweza kuibua dhamira za msanii katika utanzu huu wa riwaya.

Hivyo basi, utafiti huu ulichunguza kwa namna gani tamathali za semi zinaibua dhamira katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Tamathali za semi ni

vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilishana maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum ya kifasihi iliyokusudiwa na mtunzi (Mulokozi na Kahigi (1979).

Kahigi (1994) anadai kuwa msingi wa tamathali za semi nyingi ni uhamishaji wa maana. Uhamishaji wa maana ni mbinu ya kuibua maana ya kiashiria (neno, fungu n.k) kutokana na maana ya kiashiria kingine. Kanuni ya jumla ya uhamishaji wa maana ya kitamathali x inachukua nafasi ya maana ya kawaida Y iwapo x inahusiana na Y kwa njia fulani.

Utafiti huu unajikita katika kuchunguza tamathali za semi ili kuona kwa namna gani tamathali hizo zinatumika kuibua dhamira. Kwa hiyo, utafiti huu unachunguza tamathali za semi ambazo kwa kawaida hujikita katika uhamishaji wa maana; kutoka katika dhana moja kwenda katika dhana nyingine ili kuwasilisha dhamira zilizokusudiwa kwa hadhira.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1979) tamathali za semi ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum ya kifasihi iliyokusudiwa na mtunzi. Kwa kifupi tamathali za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana zinazotumiwa na mwandishi ili kuibua dhamira. Suali hili linaungwa mkono na Wafula na Njogu (2007:98) kwa kufafanua kuwa, dhamira za msanii haziwezi kutenganishwa na jinsi msanii

huyu anavyoiwasilisha kazi yake. Adam Shafi kwa kiwango kikubwa ameiwasilisha kazi yake kwa kutumia tamathali za semi. Kwa hiyo, kutokana na mawazo hayo, swali la kujiuliza ni dhamira zipi zinazoibuliwa kutokana matumizi ya tamathali za semi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*? Je, tamathali za semi zinaweza kubainisha dhamira katika kazi za fasihi? Kwa hiyo, tatizo la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya tamathali za semi katika riwaya ya Shafi Adam Shafi ili kuona ni jinsi gani msanii huyo anatumia kipengele hicho cha tamathali za usemi katika kuibua dhamira zake.

## 1.3 Lengo la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya tamathali za semi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ya Shafi Adam Shafi ili kuona jinsi gani vipengele hivyo vinatumika katika kuibua dhamira za kazi hiyo.

### 1.3.1 Malengo Mahsusi

(i) Kubainisha tamathali za semi zilizotumika katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.

(ii) Kubainisha dhamira zinazoibuliwa na tamathali za semi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.

## 1.4 Mwaswali ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na maswali yafuatayo:

(i) Je, ni tamathali zipi za semi zinazotumika katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*?

(ii) Je, dhamira zipi zinazoibuliwa kutokana na matumizi ya tamathali za semi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa katika taaluma ya Fasihi. Matokeo ya utafiti huu yatachangia kupata maarifa ya ziada juu ya tamathali za semi zinavyojenga dhamira katika kazi za fasihi. Hivyo basi, utafiti huu unaweza kusaidia kufanyika kwa tafiti nyingine zaidi kutokana na mahitimisho yaliyofikiwa.Vile vile utafiti huu utaweza kutumika kama rejeleo na chachu ya tafiti nyingine katika fasihi na lugha. Aidha, mapendekezo ya tafiti zijazo katika maeneo ambayo utafiti huu haukuweza kuyagusa kutokana na malengo ya watafiti wengine ili kuzalisha tafiti nyingi zaidi katika lugha ya Fasihi.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kuchambua tamathali za semi katika riwaya ya Kiswahili. Pamoja na kuwapo waandishi wengi wa riwaya, sio jambo rahisi kuchunguza riwaya za waandishi wote, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza na kuchambua tamathali za usemi katika riwaya moja tu ya Shafi Adam Shafi. Sababu ya kumchagua Shafi ni kwa sababu ni mtunzi mwenye athari kubwa katika fasihi ya Kiswahili. Shafi Adam Shafi ametunga riwaya nyingi, miongoni mwa hizo ni: *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (1978), *Kuli* (1979), *Vuta N'Kuvute* (1999), *Haini* (2003) na *Mbali na Nyumbani* (2013).

Hata hivyo, mtafiti ameamua kuteua riwaya moja tu ya *Mbali na Nyumbani*. Hii ni kwa sababu isingekuwa rahisi kuchunguza riwaya zote alizotunga Shafi

Adam Shafi.Kwa maana hiyo kazi zake nyengine za kifasihi hazitoshughulikiwa isipokuwa riwaya iliyotajwa tu.

Aidha, kwa vile utafiti wa utafiti huu umelenga kuchunguza tamathali za semi mbali mbali zenye sifa, muundo na dhima tofauti katika kazi za Fasihi. Utafiti huu uliona kuwa hauwezi kuchunguza tamathali za semi zote bali ulijikita katika kuchunguza tamathali za semi tano tu. Hii ni kutokana na muda wa utafiti na malengo ya utafiti huu. Kwa hiyo tamathali zilizoshughulikiwa ni; tashibiha, tashihisi, takriri, methali na tanakali sauti.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Kwanza ni ugumu wa kupatikana marejeleo kama vile tasnifu na vitabu mbali mbali vinavyohusiana na mada hii. Kikwazo hiki kinatokana na kutokuwepo kwa marejeleo ya kutosha katika eneo analoishi mtafiti, katika kutatua kikwazo hiki kwanza kabisa mtafiti alitumia mitandao kwa ajili ya kupata marejeleo mbali mbali zikiwemo tasnifu, makala pamoja na vitabu mbali mbali. Mtafiti pia alitembelea maktaba kuu ya Serikali iliopo Pemba pamoja na maktaba nyengine kama ile ya Wialaya ya Wete, maktaba ya Chuo Kikuu Huria Makao Makuu Dar es Salaam; East Africana ya Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Pili ni tatizo la kifedha, kazi hii ilimlazimu mtafiti kusafiri kwenda nje ya eneo analoishi la Pemba kwa mfano Dar-es-salaam na Zanzibar ili kutafuta marejeleo zaidi hali iliyohitaji fedha nyingi. Katika kutatua kikwazo hiki mtafiti alikusanya fedha kutoka mfukoni mwake pamoja na kuomba misaada kutoka kwa wahisani mbali mbali wakiwemo ndugu, jamaa na marafiki. Aidha

mtafiti aliomba mkopo wa kifedha kutoka Islamic Bank ili kuweza kukamilisha utafiti huu.

## 1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza ni sura tangulizi ambayo inatoa utangulizi wa ujumla wa utafiti na kuibua tatizo la utafiti. Sura ya pili inachambua na kujadili mapitio ya maandiko yanayohusiana na utafiti huu na hatimae kuibua pengo la maarifa ambalo ndilo linalihamasisha nia ya kufanya utafiti huu. Aidha, katika sura hii kiunzi cha nadharia kinachoongoza uchunguzi, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huu kinajadiliwa. Sura ya tatu inafafanua na kujadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sura ya nne ndio kiini cha utafiti huu ambapo uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data na matokeo ya utafiti huu ulifanyika kwa kina. Sura ya tano imetoa muhtasari, mapendekezo na hitimisho la utafiti huu.

## 1.9 Hitimisho

Sehemu hii ni sehemu tangulizi ambayo imejadili usuli wa mada, tatizo la utafiti na malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake na namna ya mpangilio wa tasnifu utakavyokuwa. Katika sehemu inayofuata tumechambua mapitio ya kazi tangulizi ili kuona kwa undani zaidi nini kilichokwisha kusemwa au kufanyiwa utafiti na nini hakijasemwa na watafiti wengine kuhusiana na mada hii.

# SURA YA PILI

# MAPITO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii ina vipengele vikuu vitatu ambavyo ni historia ya Riwaya, mapitio ya maandiko na mkabala wa nadharia. Katika kipengele cha kwanza tumejadili historia ya riwaya. Kipengele cha pili imehusu mapitio mbali mbali ya maandiko yanayohusiana na tamathali za usemi katika tanzu mbali mbali za fasihi na hatimae kubainisha pengo la maarifa. Tatu sehemu hii imebainisha mkabala wa nadharia ya simiotiki na jinsi ilivyotumika katika utafiti huu. Na mwisho kabisa ni hitimisho.

## 2.2 Ufafanuzi wa Istilahi

### 2.2.1 Maana ya Riwaya

Hatuwezi kupata maana ya riwaya kwa kipimo cha ubainishaji wa urefu au wingi wa maneno kwa ukamilifu wa maana ya riwaya. Iwapo tutakubaliana na Mphalele (1976) ili iwe riwaya ni lazima maneno 75,000 basi tutakuwa tunaungana kwamba hakuna riwaya katika fasihi ya Kiswahili. Chua Chua (2011) anafasili kuwa riwaya ni kazi ya kubuni ya Kinathari yenye uchangamani wa fikra, msuko, mandhari na uhusika unaosawiri binadamu na maisha yake. Hii inaonesha kwamba tunapozungumzia uchangamani, ni ile hali ya kuunda kazi kisanii kwa kutumia mbinu mbali mbali za kiubunifu, na ndipo unamfanya kumfikisha msomaji na uchangamani ndio kigezo kikuu kinachotofautisha riwaya na aina nyengine za nathari.

Maelezo yaliyotangulia yanakubalika kwa maoni yetu kwa sababu yanaonesha vigezo vilivyokusanya maana ya dhana ya riwaya kwa mkusanyiko mkubwa wa wataalamu wengi kuonesha vigezo vya urefu, uhusika wa kina, uchangamano wa mtindo na uzito wa kidhamira, masimulizi kwa kugusa nyanja mbali mbali za maisha zinazohusu walimwengu na vitu vinavyowahusu.

Mawanda ya hadithi, suala la wakati na matumizi ya mandhari. Hatuna maana kuwa ni lazima pawepo na aina zote za vigezo vilivyotajwa lakini pawepo na asilimia kubwa kuikamilisha kazi hiyo. Tunakubaliana ya kuwa vigezo hivyo vitakamilisha kuijua dhana ya riwaya na kuitofautisha na aina nyengine ya nathari. Kitu kitakachotuwezesha kusema kwa mawanda mapana kuwa kitabu cha Shafi Adam Shafi cha Mbali na Nyumbani ni miongoni mwa riwaya za Kiswahili.

## 2.3 Chimbuko la Riwaya

Ndungo na Mwai (1991) wanaeleza kuwa kuzuka miji na viwanda kulistawisha uandikaji wa riwaya na usomaji kupanuka. Maendeleo katika vipengele vyote vya maisha, kama vile Kiuchumi, Kisiasa na Kijamii, yalizusha haja ya kuwa na utanuzi wa fasihi ambao uchangamano wake wa kifani na kimaudhui ungedhibiti nyanja hizi zote. Aidha mabadiliko hayo yalileta matabaka, ambapo palizuka tabaka jipya la mabwanyenye, walihodhi viwanda na nyenzo nyingine za kiuchumi. Hivyo tabaka hili lilitaka fani mpya katika fasihi kwa sababu ya kipato cha fedha za kununulia vitabu na magazeti na kupata wakati wa ziada wa kujisomea.

Fani hiyo ya riwaya ilitawaliwa na ubinafsi. Ubinafsi huu ulijidhihirisha kiitikadi, mfano wa riwaya ya Robinson Crnisoe (1719), hudhaniwa kuwa ni riwaya iliyosawiri mawazo ya juu ya kibepari, kwa kumtumia muhusika Friday ambaye alionekana bado kustaarabika. Vile vile ubinafsi ulioonekana katika kanuni za utungaji wake kwa kuepukana na kanuni za jadi.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa mageuzi ya kijamii na kisiasa yalifungamana na mabadiliko ya kiuchumi tuliyoyataja. Mataifa ya Ulaya yalianza kujitegemea kwa kuepukana na Dola iliyokuwa tukufu ya Kirumi. Hivyo, Mataifa ya Ulaya yalianza kujipambanua kiutamaduni na kisiasa pia walijenga utamaduni wao kitaifa na mifumo ya elimu. Vile vile walianza kutumia mfumo wao wa maandishi katika lugha yao. Hata misahafu ya dini, kama vile Biblia ilianza kufasiriwa kwa lugha ya Kidachi mwaka elfu moja mia tano na Thelathini na nane (1538), kila elimu ilipopanuka na ndipo watunzi walipoengezeka na hivyo kuwa hadhira nzuri ya watunzi wa riwaya.

Mulokozi (1996) anafafanua kuwa ugunduzi wa teknolojia ya upigaji chapa vitabu kwa kutumia herufi zinazohamishika, mathalan mgunduzi aitwae Gutenberg huko Ujerumani mwaka elfu moja mia nne na hamsini (1450) ulirahisisha kazi ya uchapaji vitabu, hali iliyopelekea vitabu kuwa bei nafuu na kupatikana kwa wingi.

Ndugo (1991) anaeleza kuwa kuzuka kwa viwanda kuliwafanya waandishi wengi kuandika maandiko yaliyo marefu, hali hii ilisababisha kupatikana kwa wasomaji wengi hasa wanawake ambao waliachwa majumbani baada ya

waume wao kwenda kufanyakazi viwandani. Kwa kuwa wanawake hasa wale wa tabaka la juu walikuwa na watumwa wa kuwafanyia kazi za nyumbani. Kwa hivyo kuzuka kwa riwaya tunaweza kusema kulifungamana na mfumo wa kibepari.

Ndungo na Mwai (1991) wanaeleza kuwa kuzuka kwa mitambo ya kupigia chapa, viwanda pamoja na miji, hivi vilikuwa vyombo mahsusi vilivyokuza utanzu wa riwaya. Kulikuwa na uwezekano wa kuandika maandiko marefu marefu kwa urahisi kwa kutumia mitambo ya kupigia chapa. Hali iliyofanya nakala nyingi za maandiko hayo zingalitolewa na kusambazwa kwa urahisi. Miongoni mwa riwaya za mwanzo kuandikwa kwa Kiswahili ni ile riwaya ya Uhuru wa Watumwa (1934), kilichoandikwa na Mbotela (1934), kinaeleza kwa kusimulia habari za watumwa na uhuru wake pamoja na harakati za biashara ya watumwa katika mwambao wa Afrika Mashariki. Kitabu hiki ingawa kimeandika habari za watumwa lakini kina taathira kubwa za Kikoloni.

Mashindano yaliyoanzishwa yalikuwa ni chachu ya kuanzishwa kwa riwaya ya Kiswahili. Kutokana na mashindano hayo yaliyoanzishwa na Taasisi, waandishi wengi wa Afrika walijitokeza na kuandika riwaya. Mifano ya waandishi hawa ni Shaaban Robert (1960), ambaye vitabu vyake vilichota kwa kiasi kikubwa utamaduni wa wageni, vitabu kama vile Kusadikika na Kufikirika. Ali Jemedar naye aliandika riwaya ya Nahodha Fikirini, wengine walioshiriki katika mashindano haya ni Moh’d Saleh Farsy (1960) alitoa Kitabu cha Kurwa na Doto, Mohamed Suleiman Abdalla (1960), aliandika Watu na Wanawe.

Katika maendeleo ya riwaya za Kiswahili, uandishi umepiga hatua fulani hasa baada ya uhuru, nje ya ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki, mantiki imeongezeka maradufu. Kwani maudhui, mantiki, mtiririko hata mtindo inasonga mbele kila uchao. Hivyo riwaya nyingi zimeandikwa miaka ya sabiini na thamanini. Waandishi kama vile Euphrase Kezilahabi, Said Ahmed Mohamed, Suleiman Mohamed, Mohamed Said Abdalla, ndio washika bendera kwa kuzingatia kigezo cha maudhui na uumbaji wa kisanaa.

Tunapochunguza maelezo hayo ni dhahiri kuwa chanzo cha riwaya za Kiswahili ni mchango mkubwa uliotokana na biashara na mapinduzi ya viwanda huko Ulaya. Hali hii ilianza Ulaya na kuja Afrika kwa kutumia biashara ya baharini, ambapo biashara hii ilipotokea Ulaya kuja Afrika iliathiri kwa kiasi kikubwa mila, silka na desturi za Waafrika. Hali iliyopelekea kufuta uhalisia wa Kiafrika na kuwa mchanganyiko kati ya Uafrika na Uzungu, ndipo pakapatikana kitu kiitwacho riwaya inayotokana na fasihi andishi badala ya hadithi inayotokana na fasihi simulizi.

Kutokana na uwelewa wa kina wa Riwaya na chimbuko lake, utafiti huu umeona kuwa ipo haja ya kuchunguza tamathali za semi katika kuibua dhamira katika riwaya ili kuona ni jinsi gani kipengele hiki cha fani kimeingizwa katika utanzu wa riwaya kama mbinu ya kisanii inayotumika kujenga riwaya za Kiswahili.Kwa hiyo, utafiti huu ulichunguza tamathali za semi katika kuibua dhamira katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.

## 2.4 Maana ya Tamathali za Semi

Tamathali za semi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii ili kutia nguvu katika maana, mitindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Wakati mwengine hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha (Senkoro, 1984). Hii ina mana kwamba ili msomaji wa kazi yoyote ya fasihi apate ujumbe hana budi kufikiri kwa kina.

Msokile (1992) anaeleza kwamba, tamathali za usemi ni fungu la maneno lililoongezwa maana yake kamili ili kuiwakilisha maana nyingine. Akiwa na maana kuwa katika tamathali zipo maana na matumizi mengine ya kisanii ambayo msanii anapaswa kuyatumia ili aweze kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.Mwamanda (2008), yeye anaeleza tamathali za usemi ni viwakilisho na vifananisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti zinazofanana. Huu ni usemi unaobadilisha maana dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya fasihi iliyokusudiwa na msanii.

Kutokana na fasili hizo za tamathali za usemi, tunaona kuwa kwa ujumla tamathali za usemi ni maneno au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii au waandishi wa kazi za fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti za kusema au maandishi. Aidha tamathali za usemi hutumika katika fasihi kwa lengo la kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu katika lugha iliyotumika katika kazi husika. Tamathali hizi huweza kugawanyika katika vipengele tofauti tofauti kama vile tamathali za mlinganisho, tamathali za mafumbo, tamathali za msisitizo pamoja na tamathali nyingine za usemi.

Vipengele vya tamathali za usemi ni muhimu sana katika kuunda au kutoa msisitizo wa maana pamoja na kuunda maana mpya katika kazi za fasihi. Hivyo mtafiti alichunguza tamathali za usemi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ili kuona zinavyoibua dhamira katika kazi ya fasihi.

## 2.5 Tafiti Kuhusu Riwaya za Shafi Adam Shafi

Katika sehemu hii tunapitia kazi tangulizi juu ya riwaya za Shafi Adam Shafi ili kubaini watafiti na wahakiki watangulinzi wamezungumza nini kuhusu kazi hizo na kubainisha pengo la kiutafiti ambalo linahitaji kujazwa na utafiti huu tuliofanya. Kimsingi, wapo watafiti na wahakiki kadhaa ambao wamechunguza na kueleza juu ya kazi za Shafi Adam Shafi kwa namna mbali mbali kulingana na madhumuni ya kazi zao. Khatibu (1983) alifanya uhakiki wa riwaya ya *kuli* na kueleza kuwa dhamira kuu katika riwaya hiyo ni ukombozi wa kitabaka. Ukombozi huu ulikuwa unafanywa na watu wa tabaka la chini dhidi ya tabaka la juu kuhusu mgawanyo sawa na sahihi wa rasilimali za taifa. Mhakiki anaeleza kwamba, Serikali ya Kikoloni iliwatesa na kuwatumikiha wananchi wa Zanzibar kwa maslahi mapana ya Wakoloni huku wakiishia kuwa katika maisha duni kabisa.

Khatibu (ameshatajwa) hakuchambua kwa kina juu ya dhamira za riwaya hii na badala yake ameishia kutaja tu na kueleza kwa ufupi. Hata hivyo, maelezo yake kuwa, "ukombozi ulikuwa unafanywa na watu wa tabaka la chini kuwashusha watu wa tabaka la juu", yamekuwa na umuhimu mkubwa katika kutufahamisha ni ipi dhamira kuu katika riwaya ya *kuli* na kutuwia rahisis sisi kufanya uchambuzi wa kina kuhusu riwaya hii katika dhamira husika.

Mulokozi (1990) aliandika makala juu ya utunzi wa riwaya ya kihistoria ya Kiswahili na kueleza mambo mbali mbali ya kifani na kimaudhui yanayoipamba riwaya hiyo. Katika harakati zake za kukamilisha lengo hili alimtaja Shafi Adam Shafi kuwa ni miongoni mwa waandishi ambao wanatunga riwaya ya kihistoria. Amelisema hili kwa kutolea mfano kuwa ujenzi wa wahusika katika riwaya za mtunzi huyu zinaashiria kwamba, yeye ni mtunzi wa riwaya za Kihistoria.

Kimsingi, mfano unaotolewa na Mulokozi (ameshatajwa) tunakubaliana nao kwani hauna shaka kuwa riwaya karibu zote za mtunzi huyu zimeandikwa katika muktadha wa Kihistoria. Kwa mantiki hiyo, mafunzo tuliyoyapata katika makala ya Mulokozi yametufungua macho ya kuzielewa vizuri riwaya za Shafi Adam Shafi kuwa ni za kihistoria na pale tunapozichambua tunalizingatia hili.

Hata hivyo, maelezo ya Mulokozi ni ya kiudokezi tu na hajazama katika kina kirefu cha uhakiki wa riwaya hizo. Utafiti huu umefanywa kwa kuzama ndani na kuchambua mambo mbali mbali katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ya Shafi Adam Shafi. Njogu na Chimerah (1999) waliandika kitabu ambacho walikiita *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu* ambacho kimesheheni hazina kubwa ya masuala ya fasihi ya Kiswahili na ile ya makabila mengine ya Kafrika.

Katika kitabu hiki wametoa darasa la kutosha kwa walimu, wahadhiri na wote wanaohusika na ufundishaji wa fasihi juu ya namna bora ya kufundisha kazi za fasihi katika ngazi hizo wanazofundisha. Kwa mfano, kila kipengele kiwe ni cha fani au kimaudhui kimeelezwa vile kinavyopaswa kufundishwa darasani ili wanafunzi

waweze kuelewa. Katika kutoa mifano mbali mbali ya kukamilisha hoja zao, wamekuwa wakitolea mifano riwaya za Shafi Adam Shafi kuhusu *Kasiri ya Mwinyi Fuadi* na *Kuli*. Mifano hiyo imekuwa ikihusu vipengele vya kifani na kimaudhui.

Kimsingi, maelezo ya kiufundishaji wa fasihi darasani yanayotolewa na wawili hawa yamekuwa na umuhimu mkubwa katika kupeleka mbele utafiti wetu. Mawazo yao yametusaidia sana katika kufanikisha uchambuzi na uhakiki tulioufanya katika sura ya nne ya tasnifu hii.Mtaalamu mwengine alieandika kuhusu riwaya za Shafi Adam Shaf ni Wamitila(2002 ambapo alieleza kuwa Shafi Adam Shafi ni mtaalamu sana katika matumizi ya mbinu ya kueleza sifa za wahusika wake pamoja na wasifu wao.

Anaeleza kwamba mbinu hii ni nzuri kwa sababu humfanya msomaji kuwaelewa vizuri wahusika wa riwaya hizo na kisha kuweza kuhusisha vyema matendo yao na wasifu wao. Hili linapotokea inakua ni rahisi sana kwa msomaji kuipata dhamira iliyokusudiwa na muandishi. Katika kusisitiza hoja yake, Wamitila (ameshatajwa) anatolea mfano namna Shafi Adam Shafi anavyompamba Yasmini kwa sifa mbalimbali za uzuri kwa kutaja wasifu wake ambao unapatikana katika ukurasa wa kwanza wa riwaya ya *Vuta Nkuvute.*

Pia, Wamitila (2008) aliandika kitabu adhimu katika taaluma ya fasihi na kukipa jina la *Kazi ya Fasihi.* Katika kitabu hiki amehudhurisha vipengele mbali mbali ambavyo vinajenga kazi mbali mbali za fasihi na namna ya kuvichambua au kuvihakiki vipengele hivyo kitaaluma. Vile vile ametaja na kutoa ufafanuzi kuhusu mbinu mbali mbali za usomaji wa kazi za fasihi ili kuwawezesha wasomaji kupata yale wanayoyahitaji kama wanavyo yahitaji kutoka katika kazi mbali mbali za

fasihi ambazo watazisoma kwa makusudio mbali mbali. Kazi hii ya Wamitila (ameshatjwa) ni muhimu sana katika kupeleka mbele utafiti huu wetu ambao umechunguza tamathali za semi katika riwaya ya *Mbali* na *Nyumbani.*

Maelezoya mtaalam huyu yametusaidia kufahamu nanma ya kuzipata dhamira katika kazi za riwaya pamoja na namna ya kutambua vipengele mbali mbali vya kisanaa vinavyotumiwa na watunzi wa kazi za fasihi katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira iliyokusudiwa. Tunasema hivi kwa sababu katika kutoa mifano ya kuthibitisha mawazo yake Wamitili (2008) amekuwa akirejelea hapa na pale riwaya za Shafi Adam Shafi hususan *Kasiri ya Mwinyi Fundi, Kuli, Vuta N'kuvute* na *Haini.*Kutokana na kuzitaja riwaya hizi na kuonesha namna mbinu mbalimbali za kisanaa zinavyojitokeza imekuwa ni rahisi kwetu kuzipata mbinu hizo na kisha kufanyia uchambuzi wa kina tofauti na yeye alivyofanya katika kitabu chake.

Diegner (2011) alifanya mazungumzo na Shafi Adam Shafi kuhusu uandishi wake wa riwaya tangu alipoanza mpaka hapa alipofikia. Katika mazungumzo yao alimuuliza maswali mengi kuhusu mambo yaliyomsukuma mpaka akaandika riwaya alizoziandika. Bila choyo Shafi Adam Shafi amejibu maswali aliyoulizwa kwa ustadi mkubwa kiasi cha kumwezesha msomaji au mtafiti kupata mambo mengi kuhusu utunzi wa riwaya uliofanywa na Shafi Adam Shafi.

Kwa mfano, aliulizwa swali kwamba, anauelezeaje utunzi wa *kuli* na ule wa *Vuta N. Kuvute?* Jibu alilolitoa ni kwamba, Kuli ndiyo riwaya yake ya kwanza kupata kuitunga kwa hivyo hakuwa ameiva katika sanaa ya utunzi wa riwaya hali ya kuwa

alipotunga *Vuta N'kuvute* alikuwa ameiva kiasi na hivyo kutowa riwaya imara iliyopata tuzo ya uandishi bora nchini Tanzania.

Kimsingi, mazungumzo baina ya Diegner(ameshatajwa)na Shafi Adam Shafi ni muhimu sana katika kupeleka mbele utafiti wetu kwa namna mbalimbali. Kwanza kupitia mazungumzo haya tumepata data za kutosha kumuhusu mwandishi na hivyo kutokuwa na haja ya kufanya mahojiano na mtunzi wa riwaya tuliyoishuhulikia kwa sababu kila tulicho kihitaji tumekipata. Hivyo basi, muda ambao tulikua tuutumie kufanya mahojiano na mtunzi tuliutumia kufanya jambo jengine na hivyo kuweza kukamilisha lengoletu kuu la utafiti huu kwa muda muafaka.

Pili, mazungumzo ya Shafi Adam Shafi na Diegner (amesha tajwa) yamesaidia sana kupata data na kukazia au kukamilisha zile ambazo tumezipata kwa kudondoa katika riwaya husika na hivyo kujibu maswali yetu ya utafiti kwa uhakika na ufasaha zaidi. Jambo hili pia linafanya utafiti wetu kuonekana kuwa ni hai kutokana na kuwepo kwa maelezo dhahiri ya mtunzi wa riwaya tuliyoishughulikia na hivyo kumfanya msomaji kuamini uchambuzi wa data tulioufanya katika tasinifu hii.

Upatanisho wa kile kinachosemwa na mwandishi katika riwaya yake na kauli zake halisi kuhusiana na riwaya zake ni kitu muhimu sana katika kuuchambulisha utafiti husika na kuufanya utafiti wowote ule wa kitaaluma kuaminiwa na wana taaluma pamoja na wasomaji wengine wote kwa ujumla wao. Kwa hakika, mazungumzo baina ya watu hawa wawili yamekuwa na umuhimu mkubwa sana katika kukamilisha utafiti shuu kama unavyo onekana hivi sasa.

Si hivyo tu bali pia walibora (2013) ameandika makala kuhusu riwaya mpya ya tawasifu ilio andikwa na Shafi Adam Shafi juu ya maisha yake riwaya ambayo ndiyo tunayo ifanyia utafiti. Pamoja na mambo mengi aliyo yaeleza, kubwa ni kumsifu Shafi Adam Shafi kuwa ni miongoni mwa watunzi wajasiri ambao ameweza kueleza mambo mbali mbali, waziwazi yanayohusu maisha yake bila kificho. Anasema kwamba sijambo la kawaida kwa mwandishi wa kazi ya fasihi inayo muhusu yeye mwenyewe na kisha akataja mambo ambayo kwa mtazamo wa wengi yanaweza kuwa yanamuaibisha mbele za wasomaji wake. Shafi Adam Shafi ametaja mambo hayo bila woga wowote na hivyo kumfananisha na Shaaban Robert alipo andika *Wasifu wa Siti Binti Saad* na tawasifu ya maisha yake iliyoitwa *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*.

Mawazo haya yanamchango mkubwa katika kupeleka mbele utafiti wetu hususani katika kujibu maswali mawili ya utafiti wetu. Kwanza, suala la mwandishi kutunga riwaya ya tawasifu na kisha kueleza kila kitu hadharani limetufundisha jambo. Kumbe katika kipindi hiki cha utandawazi ambapo mambo huelezwa waziwazi kimefikia mpaka katika riwaya ya Kiswahili, jambo linalodhihirisha kwamba, riwaya inasawiri hali halisi ya maisha katika jamii.

Hata hivyo, kwa maoni yetu tunaona kwamba, si sahihi kwa kazi ya fasihi kueleza kila jambo kwa uwazi kwa sababu si kila jambo linapaswa kuanikwa mbele za watu. Kwa mfano, suala la Shafi kueleza kwamba, alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanawake kadhaa huko Sudani wakati wa ujana wake halikupaswa kutokea katika riwaya yake hii ya *Mbali na Nyumbani.* Hakuna asiyefahamu kwamba, kijana anapo

baleghe huwa anakuwa katika hali gani na kwa vyovyote vile atatafuta njia ya kujihifadhi.

Kama hivyo ndivyo, haikuwa na haja yeye kusema waziwazi mambo hayo kwa sababu inakuwa ni kama vile anahamasisha watu kufanya uasharati kwa kule kuonesha kwamba, hicho ni kitu cha kawaida tu. Kwa mantiki hiyo, katika utafiti wetu tumekuwa makini katika matumizi ya lugha ya uhakiki tuliofanya ili isije ikatokea tumetumia lugha ambayo si stahiki katika muktadha huu wa kitaalamu.

### 2.5.1 Tafiti Kuhusu Tamathali za Semi

Wanyonyi (2009) alihakiki riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ya Said A. Mohammed. Katika kazi yake alishughulikia matumizi ya lugha ya kitamathali kama vile tafsida, ishara za uashiriaji na maswala ya balagha. Vile vile, aliangazia kazi yake kwa mtazamo wa Saikolojia changanuzi.

Kazi hii ya Wanyonyi ilitusaidia katika kupata dira ya utafiti wetu. Aidha kazi yetu ilijikita katika riwaya ya Shafi Adam Shafi ya *Mbali na Nyumbani* ambapo tumetumia nadharia ya simiotiki kinyume na Wanyonyi ambaye ametumia nadharia ya saikolojia changanuzi.

Too (2011) alitafiti tamthiliya ya *Nguzo Mama* (1982) ya Penina Muhando. Alitumia nadharia mbili ambazo ni Umuundo na Semiotiki kuchanganulia mbinu anuai za lugha. Mbinu hizi ni pamoja na tamathali za usemi kama vile tashbiha, sitiari, chuku, majazi, tanakali sauti na mbinu nyingine za lugha. Ingawa kazi ya Too ni katika utanzu wa tamthiliya lakini imetusaidia sana

katika kubaini vipengele vya tamathali za usemi ikiwa ni sehemu ya vipengele kama hivyo ndivyo kazi hii inavyovichunguza, ingawa kazi hii imeegemea katika utanzu wa riwaya kinyume na kazi ya Too ambayo imeegemea katika utanzu wa tamthiliya. Kubwa zaidi Too ametumia nadharia ya simiotiki na umuundo wakati utafiti huu umetumia nadharia ya Simiotiki pekee kuibua na kuchambua dhamira.

Jilala (2010/2011) katika makala yake ya lugha na ujinsia katika ushairi ambapo alifanya uchunguzi wa sitiari za UKIMWI na mapenzi katika mashairi ya Bongo fleva, Jilala anajadili kuwa katika mashairi ya Bongo fleva sitiari zinazomrejelea mwanamke zimebeba dhana nne ambazo zimeundwa kitaswira kumuashiria mwanamke na nafasi yake katika jamii. Dhana hizo ni thamani, unyenyekevu, utamu na mvuto. Dhamira hizi alizoziibua zimetusaidia sana katika kujadili dhamira zinazojiibua katika tamathali za usemi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.

Kwa mujibu wa Abbas, Ramadhani (2005) alifanya utafiti wa matumizi ya sitiari katika tamthiliya ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein na *Ngoma ya Ng'wana Malundi* ya Emmanuel Mbogo. Utafiti wake ni utafiti linganishi wa kielimu mtindo ambapo alilinganisha tamthiliya mbili. Aidha alihitimisha kuwa sitiari hutumika katika ujenzi wa dhamira mbali mbali katika tamthiliya zote mbili. Hata hivyo, sisi tumechunguza dhamira zilizomo katika tamathali za usemi za katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.

Abbas (2015) alichunguza tamathali za usemi katika kuibua dhamira katika tamthiliya za *Morani* na *Fumo Liongo* za Emmanuel Mbogo ambapo aliangalia tashbiha, tashihisi, sitiari na takiriri .Utafiti wake ni utafiti linganishi ambapo alilinganisha tamthiliya hizo mbili. Mtafiti aligundua kwamba tamthiliya ya *Morani* imekuwa na matumizi makubwa zaidi ya tamathali za usemi na kuwa na mdafao mkubwa zaidi wa uibuaji dhamira ukilinganisha na tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Katika utafiti wetu, sisi tumeangalia riwaya moja tu ya *Mbali na Nyumbani* katika kuchunguza dhamira zilizomo katika tamathali za usemi tulizoziainisha.

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia

Dhana ya nadharia imeelezwa na wataalamu kadhaa akiwemo Wamitila (2002), anasema kuwa, nadharia ni kauli ya kaida za kiujumla zinazotegemezwa kwenye uwazaji fulani. Kauli au kaida hizi huweza kutumiwa wazo kuu, fikra kuu, muongozo mkuu wa mtu au jamii wa pahala na wakati. Kutokana na maelezo ya wataalamu hao inaonesha kuwa nadharia ndio msingi mkuu wa kuweza kuelezea jambo fulani ili liweze kukubalika, kuaminika na kufanyiwa kazi na watu wa jamii husika.

Kutokana na uelewa huo wa nadharia, zipo nadharia mbali mbali za fasihi zinazoweza kutumika katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti wa kazi za fasihi. Baadhi ya nadharia hizo ni; Ufeministi, umuundo, Semiotiki, mwitiko wa msomaji, sosholojia na mwingiliano matini. Hata hivyo, kufaa au kutofaa kwa nadharia moja hutegemea malengo ya utafiti. Baada ya kuzitalii nadharia hizo, mihimili ya mawazo, ubora na mapungufu yake, tuliona kuwa kulingana

na malengo ya utafiti wetu nadharia ambayo itatuongoza kufikia malengo hayo ni nadharia ya Simiotiki. Sehemu inayofuata inayojadili nadharia hiyo, sababu ya kuichagua nadharia ya Simiotiki, namna ilivyotumika kuchunguza, kuchambua na kujadili data za utafiti huu na kufaa kwa Nadharia hiyo.

### 2.6.1 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni neno la lugha ya Kiyunani lenye maana ya ishara.Nadharia hii ni nadharia iliyoasisiwa na Ferdinand desausswe (1857 – 1980). Charles Peirce (1839-1914) na Rolland Barthes (1915 - 1980). Semiotiki ni neno ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuzihakiki kazi za kifasihi ambao unaangaza ishara katika kazi hizo. Ishara zinazojitokeza katika kazi za kifasihi, huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Chandler (1992) anaeleza kuwa, binadamu ni mtengenezaji na mnyambulishaji wa alama hizo. Wasomaji na watazamaji hutengeneza maana kupitia ubunifu na tafsiri zao za alama hizo. Alama hizo zinaweza kuwa katika mfumo wa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, matendo na kadhalika. Chandler anamalizia kwa kusema, kitu chochote kinaweza kuwa alama kama watu watakifanya kirejelea chao, yaani kinasimama kwa niaba ya kitu kingine.

Wamitila (2002) anaeleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja, yaani umbo ambalo alama inachukua na kirejelea, yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo. Kutokana na maana hiyo tunapata kufahamu

kuwa, kuna kitaja na kirejelea, ambapo mhusiano wa viwili hivyo, huwa ni wakubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii inayohusika.


Ellis na Mc Clintock (1990) wanadai kuwa, wafuasi wa nadharia ya Simiotiki hutilia maanani zaidi ujumbe unavyofasiriwa kuliko vile mchakato wa uwakilishaji wa ujumbe huu unavyofanyika. Katika uchunguzi wake, mtafiti atazingatia zaidi jinsi ujumbe (dhamira) ulioko kwenye tamathali za usemi unavyofasiriwa. Hapa, zinatumiwa kama makala na nyenzo ya kifasihi yenye ishara zinazobeba dhamira fulani. Kiashiriwa + Kiashiria = Ishara.Ishara ni kitu au alama yoyote ile inayowakilisha kitu kingine.

Brown (1995) anasema kuwa, ishara hupata maana kutokana na matumizi yake. Ili watu waelewe kinachowasilishwa na ishara fulani, lazima watu hawa wawe na makubaliano fulani ambayo hutokana na kushiriki elimu, utamaduni, dini na mandhari sawa. Ishara hizi hujumuisha picha, rangi, mambo mbali mbali na hata herufi zinazounda maneno. Watu wa asili tofauti huweza kuelewa ishara sawa kwa njia sawa kutegemea tajriba zao ilhali watu kutoka jamii moja, wenye kuzungumza lugha moja na kushiriki utamaduni sawa huwa na ukubaliano kuhusu ishara fulani na maana zake.

Kimsingi tunaweza kusema basi, hii ni nadharia inayoshughulika na ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Mwelekeo mkubwa wa kazi hii wa kupendelea neno “matini” unawafanya baadhi ya wahakiki kuiita nadharia ya umatini (texttuality). Baadhi ya wahakiki kupendelea neno ‘Simiolojia’ badala ya Simiotiki. Suala la ishara na uashiriaji kama anavyoeleza Culler (1989)

limeanza kuwa muhimu katika uhakiki wa kifasihi wa miaka ya karibuni. Kwa kuliangaza suala la uashiriaji katika kazi za kifasihi, Simiotiki humulika jinsi kazi hizo zinavyowasiliana na wasomaji. Nadharia hii haisisitizi tu masuala ya kifasihi au jinsi tunavyoifasiri kazi fulani tu, bali pia usomaji wa kazi hizo na kujiuliza kwa nini kazi za kifasihi kuwa na maana zilizonazo kwa wasomaji wake.

Kuzuka kwa nadharia hii kunahusishwa kwa kiasi kikubwa na miaka ya 1970. Licha ya kuzuka kwake wakati huo, Simiotiki imefaidi kutokana na mawazo ya mwanaisimu wa Ki – Swizi Ferdinand de sau ssure (1857 - 1931), pamoja na mwanafalsafa wa Kimarekani anayejulikana kama Charles Pierce (1839 - 1914). Pierce anahusisha na kielezea cha ishara kinachohusishwa na pembe tatu.




Pierce (ameshatajwa) anaamini kuwa kila ishara ina misingi inakotegemewa ili kutafsiriwa kwake kuwezekane. Misingi hiyo huzua aina tatu za ishara kielelezi, ishara – tanakali na taashira. Kielelezi hutumiwa kuelezea uhusiano fulani kati ya ishara na kinachoashiriwa, ishara – tanakali hutumiwa pale ambapo pana uhusiano kati ya ishara na kiashiriwa. Taashira kwa upande wake hutumiwa kuelezea aina ya ishara ambayo huashiria kutokana na matumizi ya kinasibu ya kikawaida tu. Kwa kiasi kikubwa Barthes (1915 - 1980) anasifiwa

kwa kuhakikisha kuwa nadharia ya Simiotiki haikuishia kuzisambaza sifa za kitaaluma sana kama ulivyofanya umuundo. Nadharia hii hujitahidi kwa kiasi kikubwa kuvichunguza na kuvibainisha vigezo vya ufasihi wa matini za kifasihi. Lengo kuu la jitihada hii ni kuzuka na hali ambapo msomaji yoyote yule anaweza kuitambua ni matini ipi ambayo ni ya kifasihi na ipi si ya kifasihi.

Utambuaji huu unapaswa kutokana na matini yenyewe, na vigezo vya ndani. Matini ambazo hutambuliwa kama za kifasihi katika jamii au tamaduni mbali mbali huonesha sifa fulani za kimuundo ambazo ni msingi mkuu wa utambuzi huo. Baadhi ya sifa hizo ni kwamba matini ya kifasihi hujitenga kutokana na msingi fulani maalumu. Kujitenga huku kunaweza kutokana na msingi wa lugha inayotumiwa kila siku, kuwepo na usemi maalum n.k.

Pili, lugha ya kifasihi hutumia unasibishi kwa kiwango kikubwa.Mtunzi huweza kuyatumia maneno fulani akiwa na nia ya kusisitiza maana inayonasibishwa na maneno kuliko kinachorejelewa na neno lenyewe. Maana nasibishi ina uzito kuliko maana husishi. Tatu, lugha ya kiishara inaweza kuzitawala matini za kifasihi. Nne, kinachotawala katika matini ya kifasihi sio sifa za kipragmatiki kama msemaji, msemezwa au muktadha wa kimarejeleo bali hali ya lugha yenyewe.

Wana – Simiotiki wanashikilia kuwa kiashiria huweza kuwa kile kile bali kinachoashiriwa kikawa tofauti. Mfano mzuri ni tabia ya kupeana zawadi ya mvinyo kwenye jamii ya Ulaya. Zawadi hii inaweza kuwa na maana ya urafiki, ukarimu, pongezi, mapenzi au wema. Hapo kiashiria kinabakia kile kile–

mvinyo lakini viashiriwa ni tofauti – wema, pongezi, mapenzi na urafiki n.k. Huu ndio msingi wa kile kinachojulikana kama ‘polisemi’, hali ya kiashiria kimoja kuwa na viashiriwa mbali mbali katika lugha ya kawaida. Upungufu wa nadharia hii ni kuwa inachukulia kwamba ishara zote kila mahali nawakati wote zina maana.

Inapuuza hali ambapo ishara zingine huwa hazijabeba ujumbe wowote. Alivyosema Griffen (1997: 118) ni kweli kuwa, simiotiki inahatari ya kuwa juu ya kila kitu kiasi cha kupoteza uhalisia. Ingawa hivyo, nadharia hii bado ina mashiko makubwa katika fasihi hasa katika kipengele cha tamathali za usemi kwani ni wazi kuwa kila tamathali za usemi aliyoiteuwa mwandishi amekusudia kufikisha ujumbe kwa jamii. Hali hii ndio iliyotilia nguvu kutumia nadharia ya Simiotiki ili kuchunguza dhamira zinazopatikana katika semi zilizomo katika riwaya tuliyoiteuwa.

### 2.6.2 Sababu ya Kuchagua Nadharia ya Simiotiki

Baada ya kutalii nadharia mbali mbali za fasihi tumebaini kuwa nadharia ya simiotiki ndiyo inayofaa kutuongoza katika utafiti huu. Mihimili ya nadharia hii inaonekana kuwa, inaweza kutuongoza katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data za utafiti wetu. Hivyo nadharia hii tuliiona ni nadharia ambayo itaweza kutufikisha katika malengo ya utafiti wetu. Nadharia hii ilitusaidia katika kufafanua dhamira za tamathali za semi kwa kuzingatia upekee wa dhamira zilizomo kwenye tamathali za usemi kama kipengele maalum. Hapa tumechukua tamathali za usemi kama vile tashibiha, tashihisi, takriri, methali

na tanakali sauti kwa kutumia picha za kipekee za kisimiotiki na ambazozinaweza kutolewa tafsiri kwa mkabala wa kifasihi na kisimiotiki.

### 2.6.3 Nadharia ya Simiotiki ilivyotumika

Katika utafiti huu nadharia ya simiotiki ilitumika katika kubainisha tamathali za usemi katika riwaya teule. Kwa kutumia nadharia hii, tuliweza kutofautisha baina ya maneno na kauli za kitamathali na zisizo za kitamathali. Kwa kufanya hivyo, tumeweza kubaini maneno yapi ni tamathali.

Kwa hivyo katika kushughulikia tamathali za usemi kisimiotiki, maswali haya yalituongoza: Tamathali za usemi zinahusu nini? Je, maana ya tamathali za usemi hufasiriwa vipi na kwa kuzingatia nini? Aidha, mihimili ya nadharia hii ilitusaidia kubaini maneno ama kifungu cha maneno ni aina gani ya tamathali ya usemi kwa kuzingatia muundo, dhima na maana yake. Nadharia hii pia imetumika katika kubaini maana zilizobebwa na aina fulani ya tamathali za usemi na hivyo, tuliweza kubaini dhamira zinazoibuliwa kupitia tamathali za usemi zilizobainishwa.

### 2.6.4 Kufaa kwa Nadharia Iliyotumika

Nadharia ya Simiotiki ndiyo iliyotumika katika kuchambua data kupitia misimbo yake kama vile msimbo wa kihemetiki, kiishara, kirejelezi, matukio na kiseme. Misimbo hii ilisaidia katika kuchambua dhamira zilizojitokeza katika tamathali za usemi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ya Shafi Adam Shafi pamoja na matumizi ya lugha katika kuibua dhamira hizo. Hivyo, msanii amefaulu katika kutoa ujumbe kwa hadhira husika.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imepitia na kujadili juu ya maandiko mbali mbali kuhusu maana ya riwaya, chimbuko la riwaya, maana ya tamathali za semi, tafiti kuhusu riwaya za Shafi Adam Shafi. Pia tumezungumzia tafiti mbali mbali zilizofanywa kuhusiana na tamathali za semi, tumejadili nadharia ya Simiotiki ambayo ndiyo iliyoongoza utafiti wetu na hatimae kuibua pengo la kimaarifa ambalo utafiti huu ulikusudia kuliziba. Hivyo basi, sura inayofuata inabainisha na kuchambua mbinu za utafiti zilizotumika kukusanya data za utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti ni njia zinazotumiwa na mtafiti kukusanya na kuchambua data zitakazomwezesha kufikia lengo la utafiti wake (Enon, 1998). Sehemu hii itajadili juu ya mkabala wa utafiti . Sehemu hii imegawika katika vipengele vikuu vinane; kipengele cha kwanza kinahusu eneo ambalo utafiti ulifanyika, kipengele cha pili usanifu wa utafiti, kipengele cha tatu kundi lengwa, kipengele cha nne sampuli nausampulishaji, kipengele cha tano ukusanyaji wa data, kipengele cha sita kinahusu mbinu zilizotumika katika kukusanya data, kipengele cha saba uchambuzi wa data na mwisho tumetoa hitimisho la sura hii.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni pahala ambapo mtafiti atakwenda kutafuta na kukusanya data za utafiti wake. Hivyo, utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Chuo Kikuu Huria tawi la Pemba, Maktaba kuu ya Pemba na Maktaba ya Wilaya ya Wete. Aidha mtafiti alikwenda Dar es-salaam katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Makao Makuu pamoja na Chuo Kikuu cha Dares Salaam Maktaba ya East Africana. Mtafiti ameteua maeneo haya ya utafiti kwa sababu zifuatazo; kwanza kwa kutumia Pemba kama eneo la utafiti tuliamini kuwa itakuwa rahisi kuwapata wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria wanaosoma fasihi ya Kiswahili na wale ambao tayari wameshahitimu kutoka vyuo tofauti katika fani ya fasihi.

Hivyo wanafunzi na wahitimu hawa walirahisisha katika upatikanaji wa data kutokana na mchango wao wa mawazo bila ya kutumia gharama kubwa. Pia kwa kutumia maktaba zilizopo Pemba ilirahisisha upatikanaji wa vitabu ambavyo vilimpatia mtafiti data kwa gharama nafuu. Aidha, kwa upande wa Dar –es-salaam ni eneo ambalo kuna Maktaba zinazokidhi mahitaji ya utafiti; upatikanaji wa vitabu, wataalamu wa fasihi ya Kiswahili ambao pia waliweza kumpatia mtafiti data za kutosha alizozihitaji mtafiti katika kazi yake hii.

### 3.3 Usanifu wa Utafiti

Mtafiti alihitaji kuwa na mpango kabla ya kwenda kukusanya data. Huu si mpango kazi tu, bali ni mpango kamili unaobainisha mtiririko wote wa utafiti tangu mwanzo wa utafiti hadi mwisho. Ikumbukwe kuwa usanifu wa utafiti si njia za utafiti, na usanifu wa utafiti hutumia njia mbali mbali za kukusanyia data. Hii ina maana kwamba kabla ya kuanza kuandaa njia za utafiti ni muhimu kuwa na umbo la utafiti wenyewe unaohitaji kuufanya. Usanifu ndio utakaopima ubora wa utafiti, kwani utafiti hutathmini ubora na udhaifu wa njia za utafiti. Usanifu wa utafiti unaweza kuwa ni wa uchunguzi, mwaswali ya hojaji, kusaili kuchunguza na kuchambua data (Kothari 1985).

#### 3.3.1 Umuhimu wa Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti hurahisisha kazi ya utafiti kwani huonesha kila ngazi ya utafiti na vitu vinavyopaswa kufanywa kwa kinagaubaga. Katika usanifu wa utafiti mtafiti anabainisha njia za ukusanyaji wa data na mbinu za uchambuzi wa data zilizokusanywa. Mtafiti anapaswa kuanza kuandika usanifu kabla ya kuanza kazi ya utafiti. Usanifu uliobora ni ule unaolenga kutatua au kubainisha

tatizo la utafiti au nia ya utafiti, kwa kuangalia namna ya kupata taarifa, kubainisha ujuzi wa mtafiti katika kukusanya na kuchambua data, madhumuni ya nia kuu ya utafiti kuwekwa wazi na kwa mantiki sahihi na mipango sahihi ya upatikanaji wa muda na fedha za kufanyia utafiti.

### 3.4 Kundi Lengwa

Kulingana na (Kothari, 2004; Bryman, 2004; Kombo na Tromp, 2006), kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti. Cooper (1989 na Vans (1990), wanaeleza kuwa kundi lengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au element ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni pamoja na wanafunzi wa Uzamili katika fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria tawi la Pemba, wahitimu wa kozi ya Uzamili waliosoma vyuo mbali mbali. Kwa upande wa wanafunzi wa Uzamili wanaosoma Chuo Kikuu Huria mtafiti aliwateua kulingana na madhumuni maalum, kwa kigezo kuwa ni wanafunzi wanaosoma fasihi, wana maarifa ya kutosha ya nadharia ya uchambuzi wa kazi za fasihi na pia wana ujuzi na maarifa katika matumizi ya nadharia na mbinu za uhakiki wa kazi za fasihi.

Aidha wanafunzi wa Uzamili katika fasihi ya Kiswahili wa fasihi Chuo Kikuu Huria ni kwamba watapatikana kwa urahisi.Pamoja na hayo, itakuwa rahisi kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria kwa sababu wako karibu na kuna eneo maalumu la kuweza kuwapata kwa vile kuna eneo mahsusi walilojiwekea kukutana siku moja ya kila wiki. Wahitimu wa kozi ya Uzamili ni kundi muhimu katika utafiti huu, kwa sababu wao wana ujuzi na maarifa ya kutosha

katika nadharia na vitendo kuhusu fasihi ya Kiswahili na uhakiki wa kazi za fasihi kwa ujumla. Pia kundi hili lina uzoefu wa kutosha katika kazi za utafiti. Hivyo kwa kutumia kundi hili tuliweza kupata data za kutosha kuhusu Shafi Adam Shafi kutokana na kitabu chake teule *Mbali na Nyumbani* katika utafiti huu, wataalamu hao ni kundi muhimu katika utafiti huu kwa sababu wao wana ujuzi na maarifa ya kutosha katika nadharia na vitendo kuhusu fasihi ya Kiswahili na uhakiki wa kazi za fasihi kwa jumla. Hivyo kwa kutumia kundi hili tuliweza kupata data za kutosha kuhusu mada za utafiti wetu.

Hata hivyo, pamoja na msaada wa kimawazo na kifikra kwa wanafunzi na wahitimu wa kozi hii, kwa kuwa utafiti wetu ni wa maktabani, kwa kiwango kikubwa kundi lengwa imekuwa ni msanii Shafi Adam Shafi na riwaya yake ya *Mbali na Nyumbani*.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli inatafsiriwa kama kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kutoka katika idadi kubwa ya wanajamii ama vitu vyovyote vile ambavyo mtafiti anataka kuvitafiti (Keys, na Wenzake, 1989).

Pia Enon (1998), anaeleza kuwa Sampuli ni sehemu inayoteuliwa kutoka kwenye kundi kubwa la watafitiwa ili kuwa ndio kiwakilishi cha kundi hilo. Kwa mantiki hiyo, wanafunzi wa Uzamili katika fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria tawi la Pemba,wahitimu wa kozi ya Uzamili na Wataalamu wa fasihi ya Kiswahili wa Chuo Kikuu Huria Dar es Salaam ni sehemu ya sampuli katika utafiti huu. Pamoja na makundi hayo, katika utafiti huu riwaya ya *Mbali na Nyumbani*

imeteuliwa na mtafiti ikiwa kazi teule. Mtafiti ameteua riwaya ya Mbali na Nyumbani ya Shafi Adam Shafi kwa sababu ni miongoni mwa riwaya ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kina hususan kwenye tamathali za semi.

## 3.6 Aina ya Data

Ukusanyaji wa data ni hatua muhimu sana katika kazi ya utafiti. Kabla ya kuanza kukusanya data mtafiti anapaswa kujua ni aina gani ya data anazohitaji kuzikusanya na je, data anazozikusanya zinatosha kukidhi hitaji lautafiti wake. Sehemu hii mtafiti amebainisha aina za data alizozikusanya kwa ajili ya utafiti huu. Data zilizokusanywa katika utafiti huu ni data za aina mbili: Data za msingi na data za upili.

### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi hukusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwengine yoyote yule kwa minajili kama ya utafiti huo unaofanyika hivi sasa (Kothari, 2008). Katika utafiti huu data za msingi zimekusanywa kutoka katika riwaya ya Shafi Adam Shafi ya *Mbali na Nyumbani*. Data hizi zimekamilishwa na data za upili zilizokusanywa katika vyanzo kadhaa kama inavyoelezwa hapo chini.

### 3.6.2 Data za Upili

Hizi ni data ambazo ni za kazi tangulizi na ambazo mtafiti amezipata kutoka katika Maktaba au sehemu nyengine yeyote. Data hizi ni zile ambazo watafiti wengine wameshatafiti na kuandika kuhusu mada inayotafitiwa.Mtafiti ameweza kusoma kwa undani kabla na wakati wa kufanya utafiti. Makala haya yanatoka

katika vitabu, matini, nyaraka, majarida na tasnifu mbali mbali kutoka katika maktaba.

Data za upili kwa kifupi, ni data ambazo zipo tayari bila ya kujali zilikusanywa lini na wapi. Kwa hiyo data za upili zimetumika kama marejeleo ya utafiti. Kwa hali hiyo data hizo zimekuwa ni zana za kujaribia ugunduzi wa mtafiti. Pia data za upili zimetumiwa na mtafiti kama chanzo cha taarifa (Kothari, 1985; Sarantakos, 1993).

Faida za data za upili ni kuwa ni za uhakika na ni rahisi kuzipata. Kwa kutumia data za upili mtafiti amepanua wigo wa hazina ya maarifa ambazo mtafiti ameweza kupata mawazo ya ujumla yenye ulimbe uliofanyiwa utafiti. Licha ya hayo data za upili zilimsaidia mtafiti kuthibitisha matokeo ya data za msingi.

Matatizo ya data za upili ni kuwa data zilizopo zinaweza kushindwa kukidhi mahitaji maalum ya utafiti. Wakati mwengine data zilizopo zinaweza zisiwe sahihi kama zinavyotarajiwa na kupotosha utafiti. Mara nyingine data za upili zinakuwa zimepitwa na wakati au kutokuwepo kabisa kwa watafiti wote, kwa hali hiyo kusababisha mwingiliano wa uhalisia wa taarifa. Mtafiti alitumia data za upili kutoka kwa waandishi mbali mbali ili kucha mbua usahihi wa kumbo zilizotafitiwa.

### 3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Sehemu hii ndiyo ambayo inawasilisha mbinu tulizozitumia katika kukamilisha utafiti huu. Kothari (1992) anaeleza kwamba, utafiti wa kitaaluma ni lazima

ufanywe kwa kuzingatia mbinu, njia na taratibu zote za utafiti ili uweze kupata matokeo yasiyo na shaka kulingana na kile kilichokusudiwa kutafitiwa. Kwa kuwa utafiti wetu ni wa kitaaluma tulilazimika kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba, tunatumia mbinu sahihi za kuongoza utafiti huu katika kukusanya data tunazozihitaji. Ukusanyaji wa data ni zoezi linalohitaji mbinu muafaka zinazokubalika kutokana na utafiti husika. Bila ya matumizi ya mbinu stahili data makini za utafiti haziwezi kupatikana. Hivyo, katika kukusanya data za utafiti huu mbinu ya usomaji wa machapisho imetumika.

### 3.7.1 Mbinu ya Usomaji Machapisho

Mbinu hii huhusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa na maandishi au mazungumzo (kama ilivyonukuliwa na Jilala 2014). Mbinu hii imeambatana na usomaji na uchambuzi wa matini ya *Mbali na Nyumbani*. Kazi hii ilifanyika ili kupata data zinazohusiana na tamathali za usemi zilizotumika katika riwaya husika.

Mbinu ya usomaji machapisho ilichaguliwa na mtafiti ili kupata data ambazo zilipatikana katika machapisho mbali mbali, kama vile Kitabu teule, majarida, pamoja na tasnifu zinazohusiana na mada yetu. Mtafiti alipata data za tamathali za usemi kwa kusoma riwaya ya *Mbali na Nyumbani* kwa kuzingatia sifa za kimuundo, dhima na maana katika kubaini tamathali hizo. Tamathali hizo za usemi tumezinukuu na kuzichambua kulingana na maswali ya utafiti ili kutimiza malengo ya utafiti huu.

### 3.7.2 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu

Uteuzi kwa kigezo cha madhumuni maalumu,ni uteuzi wa kuzingatia sababu mahsusi.Kombo na Tromp (2006) wanasema,ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi,hulenga kuteua kundi la watu ambao anafikiri kuwa ni rasilimali inayotegemewa katika utafiti wake.Kwa hiyo mbinu hii ni muhimu katika utafiti kwa sababu baadhi ya watu katika kundi lengwa walionekana kuwa na uwezo na ni rasilimali kubwa zaidi katika kutoa data za utafiti huu kuliko wengine.Kwa mfano,suala la kiwango cha ufahamu wa fasihi,nadharia na uhakiki kati ya wanafunzi wanaosoma fasihi na wale wasiosoma fasihi,kati ya wataalamu wanaofundisha fasihi,hususan riwaya.

Katika uteuzi wenye madhumuni maalumu, uteuzi hufanywa kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinahusiana na maswali ya utafiti kuliko kigezo cha uteuzi nasibu au wa kubahatisha.Katika mbinu hii,wahojiwa waliteuliwa kwa madhumuni maalumu kutokana na nafasi zao kwa kujuwa kuwa wao ndio raslimali ya jamii ya data za utafiti.

Kwa jumla, mbinu ya uteuzi kwa madhumuni maalumu, ilimsaidia mtafiti kupata kundi la watu wenye uzoefu,stadi na maarifa katika nadharia na uhakiki wa fasihi na riwaya na hatimae kupata data ambazo ni muhimili wa utafiti huu.Vile vile data zilizopatikana katika makundi hayo zilimsaidia mtafiti kupata na kufanya majumuisho mahsusi aliyoyakusudia kulingana na madhumuni ya utafiti.

## 3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Ili kufanikisha malengo ya utafiti wetu tulilazimika kufanya uchambuzi wa data tulizokusanya. Kothari (2008) anaeleza kwamba uchambuzi wa data ni

hatua muhimu katika kukamilisha utafiti husika.Ni katika hatua hii ndipo utafiti hukamilika na kuonekana kuwa umeweza kufanikisha lile lililodhamiriwa na mtafiti.

Utafiti huu umetumia mbinu ya uchambuzi wa data wa kimaelezo kama ilivyoainishwa na Creswell na wenzake (2006). Mkabala huu unamtaka mtafiti kutoa maelezo kwa kila data yake kwa namna ambayo inajibu maswali ya utafiti wake. Kwa mfano katika utafiti huu uchambuzi wa data umefanywa kama ifuatavyo:

Kwanza, tulianza kwa kuteua aina za tamathali za usemi ambazo tumezitumia katika kuchambua data za utafiti wetu na idadi ya kila moja ilivyojitokeza katika riwaya hiyo. Baada ya hapo tumechambua dhamira zinazojitokeza katika tamathali za usemi hizo tulizoziorodhesha. Uchambuzi huo tuliufanya kwa kutoa maelezo kwa kila tamathali ya usemi kwa namna ilivyowezesha kujibu maswali ya utafiti wetu. Tumetalii na kurejelea riwaya ya *Mbali na Nyumbani* na kisha tumerejelea maoni ya wasomi wengi waliochangia mawazo na maoni kuhusu tamathali za usemi na jinsi zinavyofikisha dhamira. Uchunguzi wetu ni wa maktabani ingawa pia tuliwashirikisha baadhi ya wanazuoni wa fani ya fasihi ya Kiswahili ili kupata maarifa zaidi kuhusiana na utafiti wetu.

## 3.9 Hitimisho

Sehemu hii imejadili kuhusiana na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji ambapo sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni

riwaya ya *Mbali na Nyumbani* kwani ni riwaya ambayo ilikidhi mahitaji ya utafiti huu. Aidha katika sehemu hii tumejadili mbinu za ukusanyaji wa data ambapo mbinu ya usomaji wa machapisho imetumika katika utafiti huu.Sura inayofuata tutajadili uwasilishaji na uchambuzi wa data. Mwisho sehemu hii ilijadili mbinu za uchambuzi wa data ambapo katika utafiti huu mbinu ya maelezo ndio iliyotumika kuchambua data za utafiti huu. Sura inayofuata itajadili uwasilishaji na uchambuzi wa data.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua data zilizopatikana katika utafiti huu kuhusiana na mada iliyofanyiwa uchunguzi. Lengo la utafiti huu ulikuwa ni kuchunguza dhamira katika tamathali za usemi katika riwaya ya Mbali na Nyumbani. Malengo mahsusi yalikuwa:

(i) Kubainisha tamathali za usemi zilizotumika katika riwaya ya Mbali na Nyumbani.

(ii) Kubainisha dhamira zinazoibuliwa na tamathali za usemi katika riwaya ya Mbali na Nyumbani.

Ili kutimiza madhumuni haya, maswali mawili yaliulizwa na kupata data toshelevu.Maswali hayo yalikuwa:

(i) Je, ni tamathali zipi za usemi zinazotumika katika riwaya ya Mbali na Nyumbani?

(ii) Je, ni dhamira zipi zinazoibuliwa kutokana na matumizi ya tamathali za usemi katika riwaya ya Mbali na Nyumbani?

Kwa ujuml wa sura hii inajibu maswali hayo mawili ambayo yaliongoza utafiti huu. Uwasilishaji, uchambuzi wa data na mjadala wa matokeo katika utafiti huu vimepangwa kwa kufuata mtiririko wa malengo mahususi na maswali yake. Sehemu ya kwanza inaangalia tamathali za usemi zinazojitokeza katika riwaya

ya Mbali na Nyumbani. Sehemu ya pili ni dhamira zinazoibuliwa katika tamathali za usemi tulizozianisha.

## 4.2 Muhtasari wa Riwaya Teule

Sehemu hii inalenga kutoa muhtasari wa riwaya iliyotumika katika utafiti huu. Lengo ni kuielezea kwa muhtasari ili kuitambulisha. Sehemu ifuatayo inatoa muhtasari wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani.*

### 4.2.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Mbali na Nyumbani*

*Mbali na Nyumbani* ni riwaya ya kitawasifu inayosimulia ari ya Shafi Adam Shafi ya kuisaka elimu. Shafi Adam Shafi katika maisha ya kiuhalisia anatoka nyumbani kwa Zanzibar akiwa amefumwa na mkuki wa kiu ya elimu. Anapofika Bunguma anaselelea. Anafanya kila kinachofanywa na kijana wa rika lake katika harakati za kuendesha maisha yake. Kisha anatumia ujanja wake wa kuvuka mpaka na akajipata nchini Uganda. Anapofika Khartoum karibu tamaa ya kuendelea na safari inamuondokea. Kula ni kwa nadra na kulala ni taabu tupu. Hatimae anajipata Kairo katika harakati ambazo hakuzitarajia, katika mafunzo ya kijeshi.

Aidha, Shafi anaporudi Zanzibar, nyumbani hapamweki. Mara hii anajipata Ujerumani kwa ufadhili wa Kisiasa, ambako nako pia panamkaa. Mbali na Nyumbani ni kisa cha matukio halisi lakini chenye msuko wa kiriwaya na chenye sifa zote za riwaya.

### 4.2.2 Maudhui katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani

Katika kazi yoyote ya sanaa, msanii anakuwa na malengo yake makuu ambayo hutaka kuyawasilisha kwa jamii husika. Hivyo basi,Shafi Adam Shafi naye pia kama wasanii wengine katika kazi yake hii ya sanaa amekusudia kuionesha jamii juu ya mambo ambayo inapaswa kuyazingatia katika kufikia mafanikio ya jambo lolote lile ambalo mwanadamu anakabiliana nalo. Kwa mantiki hiyo, katika utafiti wetu tumegundua maudhui makuu matatu ambayo msanii ameyawasilisha katika kazi yake ambayo ni;ugumu katika upatikanaji wa elimu,ustahamilivu na ujasiri pamoja na uzalendo.

## 4.3 Wasifu wa Mwandishi

Shafi Adam Shafi alizaliwa mwaka 1940 mjini Zanzibar, alipata elimu yake ya Msingi hapo hapo Zanzibar. Baada ya kumaliza elimu ya Msingi alijiunga na Chuo cha Ualimu cha Sayyid Khalifa kuanzia 1957 hadi 1960 ambacho chuo hicho baadae kilijulikana kwa jina la Chuo cha Ualimu cha Nkrumah. Alipata Diploma ya juu katika fani ya Siasa ya Uchumi katika Chuo cha FRITZHECKERT huko Ujerumani katika mwaka 1963. Sambamba na hayo alipata mafunzo ya Uandishi wa habari mjini Prague nchini Czechoslovakia katika mwaka 1964 hadi 1965, aliendelea na mafunzo hayo nchini Sweden mwaka 1982 na nchini Marekani mwaka 1983.

Aidha, Shafi aliwahi kushika nyadhifa mbali mbali za kitaaluma, akiwa Mwenyekiti wa Umoja wa waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA) kuanzia mwaka 1998 hadi mwaka 2002, pia alichaguliwa kuwa mwenyekiti

wa Baraza la Maendeleo ya Kiswahili Tanzania katika mwaka 2004. Shafi Adam Shafi ni mwandishi mwenye tajriba katika utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Anayoyasema yamempitikia, ameyashuhudia, ameyahisi na yamemfika, ama katika ndoto au katika hali halisi. Hivyo basi, Shafi ni mwandishi aliyebobea katika fani ya uandishi wa fasihi hasa hasa katika uandishi wa riwaya. Vitabu vyake alivyoandika Shafi ni kama vile: Kasri ya Mwinyi Fuadi (1978), Kuli (1979), Vuta N'kuvute (1999), Haini (2003) na chengine ni Mbali na Nyumbani (2013) kitabu ambacho mtafiti amekifanyia utafiti.

Sehemu inayofuata tutaendeleza kuhusu usimulizi katika riwaya ya Shafi Adam Shafi.

## 4.4 Usimulizi katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani

Katika kazi yoyote ile ya kifasihi, kuna kisa au hadithi fulani ambayo inasimuliwa na msimulizi. Msimulizi huyu husimulia hadithi yake hiyo kwa mtindo fulani na kwa njia maalum (Wamitila, 2002). Usimulizi katika riwaya unategemea lengo na mtazamo wa mwandhishi kuhusu jambo fulani na namna anavyotaka jambo hilo lisawiriwe au liwasilishwe mbele ya hadhira yake. Mlacha (1991) anasema kuwa mwandishi anao uwezo wa kuzungumza kuhusu wahusika wake au kupitia wahusika wake. Kwa mantiki hiyo basi, tunapata aina tatu kuu za usimulizi, ambazo ni usimulizi maizi, usimulizi wa Nafsi ya kwanza na usimulizi wa nafsi ya tatu. Shafi Adam Shafi, ametumia nafsi mbali mbali katika usimulizi wa riwaya yake ya Mbali na Nyumbani.

### 4.4.1 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza

Mlacha (1991) anaeleza kwamba, katika mbinu hii mwandishi hupotelea ndani ya mmoja wa wahusika wake ambaye husimulia hadithi yote. Shafi Adam Shafi ametumia aina hii ya usimulizi karibu sehemu yote ya masimulizi yake. Mbinu hii inajitokeza katika riwaya ya Mbali na Nyumbani ambayo tumeitafiti na hapa tutatoa mfano wa mbinu hiyo. Anasema:

> "*Mimi mwenyewe nilifurahi sana kuwa chombo hicho kisingelifika Zanzibar…*" *(uk 23).*

Huu ni ushahidi tosha wa matumizi ya mbinu ya usimulizi wa nafsi ya kwanza katika kuwasilisha dhamira kwa wasomaji wa riwaya ya Mbali na Nyumbani. Mtunzi anatumia muhusika binafsi katika kueleza mambo namna yalivyokuwa. Matumizi ya mbinu hii ni muafaka katika kuimarisha na kukazia maelezo au masimulizi ambayo hutolewa na mwandishi – usimulizi maizi. Wasomaji hupata hisia kwamba, kumbe na muhusika naye yumo katika kushadidia hoja za hapa na pale sambamba na zile ambazo zinatolewa na msimulizi na hivyo huifanya kazi kuwa hai na yenye kuwavutia wasomaji.

### 4.4.2 Matumizi ya Nafsi ya kwanza wingi

Katika mbinu hii ya usimulizi, mwandishi anasimulia akitumia nafsi ya kwanza wingi lakini anajikita zaidi katika mhusika mmoja tu. Mhusika huyu mmoja anakuwa ni msemaji wa wahusika wengine katika kazi husika ili kuonesha kwamba, jambo analolisema halimhusu yeye binafsi bali ni la watu wengi na yeye ni mwakilishi wao tu. Shafi anaitumia mbinu hii katika riwaya yake ya

Mbali na Nyumbani ingawa ni kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na matumizi ya Nafsi ya Kwanza ambayo ndio iliyotawala katika kazi hiyo. Anatumia mbinu hii kwa nia ya kusukuma mbele dhamira, visa na matukio mbali mbali kwa nia ya kumpatia msomaji wake ujumbe maridhawa, kama inavyodhihirishwa katika mfano huu.

> "*Tulikaa bandarini ambapo tulijumuika na wasafiri wengine waliojaa pale tele. Tulichezewa na usingizi usiku kucha" (uk 223).*

Dondoo hili linaonesha matumizi ya usimulizi wa nafsi ya kwanza wingi, ambapo tunamuona muhusika – Shafi akieleza kwa niaba ya wenzake. Shafi Adam Shafi amezitumia mbinu hizi mbili za usimulizi kwa kiwango cha hali ya juu, ambacho kimesaidia kuleta upatanisho mzuri wa mawazo na mtiririko wa visa na matukio, kiasi cha kumfanya msomaji aweze kuzipata dhamira stahiki bila taabu yoyote. Matumizi ya usimulizi wa aina hii humfanya msomaji kutochoshwa na hadithi simulizi na kwa vyovyote vile hufanya kila linalowezekana ili kuhakikisha kwamba, anaisoma kazi yote ili apate maudhui na dhamira zilizokusudiwa na mwandishi husika.

## 4.5 Ubainishaji wa Tamathali za Usemi katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani

Tamathali za usemi ni vifananishi au viwakilishi vya dhana moja kwa dhana nyengine tofauti na zinazofanana. Ni usemi wenye kipanua, kupuuza, au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi, Mulokozi na Kahigi (1979). Kwa mujibu wa Wamitila (2003), tamathali (za) usemi hutumiwa kuelezea fungu la

maneno, au hata neno, ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine. Kahigi (1994) anadai kuwa msingi wa tamathali za usemi ni uhamishaji wa maana.

Aidha Mbatiah (2001), anaeleza tamathali za usemi kama ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno ili kuleta maana mpya au msisitizo. Uhamishaji wa maana ni mbinu ya kuibua maana ya kiashiria kingine. Kanuni ya jumla ya uhamishaji wa maana ni maana ya kitamathali x inachukua nafasi ya maana ya kawaida ya Y iwapo x inahusiana na Y kwa njia fualni.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa, tamathali za usemi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana moja kwa kutumia dhana nyengine tofauti au zinazofanana nazo ambazo hutumia kwa lengo la kupanua, kupuuza, kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida ili kuwasilisha ujumbe na maana iliyokusudiwa kwa hadhira. Senkoro (2012) anaainisha tamathali za usemi, kuwa ni sitiari, tashibiha, metonomia, tashihisi, majazi, ishara, taashira, na kejeli. Tamathali za usemi huweza kutumiwa katika ulinganishi wa jambo moja na jingine ama tamathali hizo zinavyotumika kuibua maudhui ya kazi za fasihi.

Katika utafiti huu, tulichunguza na kubainisha tamathali za usemi ambazo zinajitokeza katika riwaya teule. Ubainishaji wa tamathali za usemi katika muktadha wa utafiti huu ulijiegemeza katika maana ya tamathali iliyotolewa

na Kahigi (1994) na hivyo, kutumia mkabala huo katika kuzibainisha tamathali za usemi. Kwa kutumia mbinu ya usomaji machapisho, utafiti huu ulichunguza na kubainisha tamathali za usemi katika matini ya riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Kwa kufanya hivi tumeweza kubaini maneno, virai, vishazi, sentensi na vifungu vya habari ambavyo vilikuwa na sifa sawa kimuundo na kidhima na kuvipanga kama aina moja ya tamathali ya usemi. Sifa za kimaana, kimuundo na kidhima zilituongoza kubaini kuwa usemi fulani ni aina fulani ya tamathali za usemi. Kwa hiyo, sehemu ifuatayo, inawasilisha tamathali za usemi tulizozichagua zilizojitokeza katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.

Katika kuchunguza tamathali za usemi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, utafiti huu ulibaini kuwa, msanii wa riwaya hii ametumia tamathali za usemi tulizozichagua kama zinavyojidhihirisha kwenye jadweli lifuatalo:

**Jedweli Na. 4.1: Tamathali za Usemi**

| **Na** | **Tamathali za usemi** | **Idadi ya Tamathali za usemi** |
|---|---|---|
| 1. | Tashibiha | 62 |
| 2. | Tashihisi | 53 |
| 3. | Takriri | 20 |
| 4. | Tanakali sauti | 22 |
| 5. | Methali | 24 |

Chanzo: Data kutoka katika Mbali na Nyumbani, Julai, 2016.

Jadweli namba 4.1. hapo juu linaonesha idadi ya tamathali za usemi tulizozichagua ambazo zimejitokeza katika riwaya ya Mbali na Nyumbani. Kutokana na data hiyo, utafiti huu ulibaini kuwa, katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* mtunzi ametumia aina tofauti ya tamathali za usemi zikiwemo zile tulizozichagua katika utafiti wetu ambazo ni tashibiha, tashihisi, takriri,methali na tanakalisauti. Katika sehemu hii tunabainisha tamathali za usemi tulizozichagua katika riwaya tuliyoifanyia utafiti.

Katika utafiti huu tumebaini kuwa, mtunzi ametumia tamathali za semi katika kazi yake hii ya sanaa. Matumizi ya tamathali za usemi yalibainisha mtindo wa msanii huyu. Mtunzi anaonekana kuwa anaamini katika ufumaji wa lugha kisanii ni kutumia utajiri wa tamathali za usemi za lugha.

## 4.6 Ubainishaji wa dhamira katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani

Moja ya malengo mahsusi ya utafiti huu ilikuwa ni kubaini dhamira zinazoibuliwa na tamathali za usemi zilizotumika katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Ili kutimiza lengo hilo, baada ya kubaini tamathali za usemi, utafiti huu ulichunguza maana za kitamathali na dhamira zinazoibuliwa na tamathali hizo. Matokeo ya utafiti huo yalikuwa kama yanavyojidhihirisha katika sehemu zifuatazo:

### 4.6.1 Tashibiha

Ni tamathali ya usemi wa kiulinganisho unaotumia viunganishi kama vile mithili ya, kama kwamba, kama, kama vile, sawa na, na kadhalika (Mulokozi, 2002; Kahigi, 1995; Senkoro, 1982). Katika utafiti huu umebaini kuwa mtunzi

wa Mbali na Nyumbani ametumia kwa kiasi kikubwa aina hii ya tamathali ya usemi kisanii kwa lengo la kujenga Dhamira katika kazi yake. Baadhi ya tashibiha zilizojidhihirisha kujitokeza katika Riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ni kama tutakavyoichambua hapa chini.

#### 4.6.1.1 Tashibiha na Uibuaji wa Dhamira katika *Mbali na Nyumbani*

Msanii wa riwaya ya Mbali na Nyumbani ametumia tashibiha kwa kiasi kikubwa kama mbinu muhimu ya kuibua dhamira zake. Baadhi ya tashibiha zinazoakisi lengo hilo ni kama zinavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

**Jedweli Na. 4.2: Tashibiha na Uibuaji wa Dhamira katika Mbali na Nyumbani**

| Na. | Tashibiha | Dhamira inayojitokeza |
|---|---|---|
| 1. | Pale mapokezi nilikaribishwa na mwanamke wa kizungu mwenye sura jamili, macho kama ya paka. | Sifa |
| 2. | Mweupe kama joya… midomo kama zuwarde | Uzuri |
| 3. | Pasi imesimama kama makali ya upanga | Usafi |
| 4. | Hakutulia kama kuku aliyetaka kutaga | Mfadhaiko na wasi wasi |
| 5. | Mweusi kama mpingo | Dharau |
| 6. | Alikuwa anapusa kama fungo | Dharau |
| 7. | Domo la chini lilining'inia kama nanga | Dharau |
| 8. | Walikuwa wengi kama siafu | Harakati za maisha katika miji |
| 9. | Ilikwenda ipendavyo ikinguruma kama simba | Kitisho |

| | | |
|---|---|---|
| 10. | Niliwaona watu wazima wakitandikwa mikwaju kama mbuzi | Udhalilishaji |
| 11. | Chetezo kilijaa, watu waliokuwa wamebanana kama uduvi. | Matatizo ya vyombo vya usafiri |
| 12. | Macho makali kama mwanga wa kurunzi | Hasira/Umakini |
| 13. | Tulikuwa tumebanana kama dagaa kwenye kapu | Matatizo ya huduma za kijamii/usafiri |
| 14. | Nywele zake kubwa nyeusi ngumu kama makumbi alizichania kwa nyuma | Dharau |
| 15. | Walikuwa wakisukumana kwa vishindo kama ng'ombe waliofunguliwa kutoka zizini. | Matatizo ya vyombo vya usafiri |
| 16. | Matumaini mema tuliyoondokanayo Kampala yalipeperushwa huko kama vumbi lililopeperushwa na upepo mkali. | Kukata tamaa |
| 17. | Tulikaa kwenye meza yetu kama mabubu | Ukimya |
| 18. | Kituo cha basi palikuwa pamejaa watu kama utitiri | Matatizo ya usafiri |
| 19. | Tulilipita daraja la Nzoia kama umeme | Ghafla |
| 20. | Shavu lilikuwa limetuna kama mgonjwa wa jino | Matumizi makubwa ya ulevi |
| 21. | Kassim alikuwa akitupeta wa mle ndani kama mchele uliokuwa ndani ya ungo | Ubovu wa miundo mbinu ya barabara. |
| 22. | Mama Halima mnene kama pipa | Kejeli/Kukejeli |
| 23. | …. Halima mwenyewe ambaye alikuwa mwembamba kama ufito | Kukejeli |
| 24. | Meno yake meupe kama yange yange lakini yeye mwenyewe mweusi kama mpingo | Kusifia na kukejeli |
| 25. | Msururu wa abiria ulitambaa taratibu kama jongoo | Matatizo ya usafiri |
| 26. | Uso umemsawijika ulikuwa umeiva kama balungi | Hasira na ukatili |

| | | |
|---|---|---|
| 27. | Lilitupita kama upepo | Mwendo wa kasi |
| 28. | Yalikuwa yamesimama kama mnara | Utulivu |
| 29. | Tulikuwa tumesimama kama miti iliyoota ardhini | Mipangilio mibovu katika utoaji wa huduma |
| 30. | Mwembamba mweusi kama masizi | Dharau/Kudharau |
| 31. | Moyo wangu ulichanua kama ua lililonyonyotewa na umande wa alfajiri | Matumaini |
| 32. | Hapo tulikuwa kama chombo kilichopigwa na shuari baharini. | Kukata tama |

Chanzo: Data za utafiti katika Mbali na Nyumbani Julai, 2016.

Jadweli namba 4.2. linabainisha tashibiha na namna ambavyo zimeibua dhamira. Hata hivyo hizo ni baadhi tu ya tashibiha ambazo tumezichunguza namna ambavyo zinaibua dhamira katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani.*

### 4.6.2 Tashihisi

Wamitila (2003) anaelezea tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai au na uhai huwasilishwa au husawiriwa kwa namna sawa na binadamu kuvipa vitu hivyo uwezo wa kufikiri na kuhisi sawa na afanyavyo binadamu.

Kahigi (1995) anafasili tashihisi kuwa ni usemi ambao sifa ya uhai huwa imehamishiwa kwenye kitu kisicho na uhai. Aghlabu, tashihisi ni tamathali za usemi ambapo vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Mfano; Jua lilikuwa likisinzia likitaka kulala. Katika utafiti huu, matokeo yalidhihirisha kuwa mtunzi ametumia tamathali ya usemi ya tashihisi kama mbinu ya utunzi na ujenzi wa dhamira za kazi yake. Jadweli lifuatalo linathibitisha maumbo ambayo yametumika kitashihisi katika riwaya hii ya *Mbali na Nyumbani*.

**Jedweli Na. 4.3: Tashihisi na Uibuaji wa Dhamira katika Riwaya ya *Mbali na Nyumbani***

| Na. | Tashihisi | Dhamira |
|---|---|---|
| 1. | Ilikuwa imemezwa na kiza cha usiku ule | Kutokuonekana |
| 2. | Ukungu uliocheuliwa na baridi hiyo ulikuwa umeenea tele nje ya vioo vya madirisha | Baridi kali |
| 3. | Mapambazuko yalizipasua mbingu | Matumaini |
| 4. | Mlima Elgon umesimama pembeni ukiuangalia mji huo | Utulivu |
| 5. | Jua ilikuwa limeshazipasua mbingu | Matumaini |
| 6. | Kila kitu ki likuwa kikimezwa na kiza kile | Kuongezeka kwa kiza cha usiku |
| 7. | Kiza bado kikifanya ukaidi hakitaki kuondoka kuyapisha mawiyo | Kuendelea kwa usiku |
| 8. | Mji wa Bungoma ulikuwa bado umelala | Utulivu |
| 9. | Hewa ilikuwa imeshiba baridi | Uwepo wa baridi kali |
| 10. | Mwanga wake hafifu uliovuja dirishani kwa uvivu ulifika mpaka nje | Matumizi ya nishati duni |
| 11. | Uume ulihamaki kweli kweli | Hamu ya kufanya tendo la ndoa |
| 12. | Njiani akili yangu ilikuwa ikibishana | Msongo wa mawazo |
| 13. | Jua lenyewe lilikuwa chini ndo kwanza likichungulia chungulia utadhani lililokuwa likiona hayakuchomoza likaonekana | Majilio ya asubuhi |
| 14. | Ziwa lililokuwa mbele yetu lilimezwa na kiza hakuna chochote kilichokuwa kikionekana | Usiku mkubwa |
| 15. | Jua lilikuwa likisinzia likitaka kulala | Magharibi |
| 16. | Siku ilikuwa imeshafumba macho hakuna ilichoona ila kiza | Usiku kuingia/iliingiliwa na usiku |
| 17. | Magharibi ilikuja ikachungulia siku tu na mara ilipotea | Usiku ghafla uliingia |
| 18. | Jua lilituzukia mbele yetu….. Pale lilisema “mtanitambua” | Jua lilichomoza na likaanza kuwa kali |

| | | |
|---|---|---|
| 19. | Hapo, mito miwili hiyo hupeana chambi na baadae kufuatana | Makutano/Mashirikiano |
| 20. | Harufu ya chakula walichokuwa wakikila ilikuwa ikilitekenya tumbo langu | Huduma mzuri kwenye mgahawa |
| 21. | Na siku ikifumbua macho taratibu | Kuchomoza kwa asubuhi |
| 22. | Nilihisi kama tuliotemwa na kiza kilichokuwa kimetumeza | Matumaini |
| 23. | Vilisimama vijumba vya udongo vilivyosongamana kwa dhiki na udhia, kila kimoja kikimwambia mwenzake nipishe | Umasikini |
| 24. | Mara gia iliingia mara ilichomoka lilikuwa likihema na kukohoa | Ubovu/Uchakavu wa vyombo vya usafiri |
| 25. | Hewa ya pale tulipokuwapo ilikuwa imeshiba harufu ya damu | Umwagikaji wa damu |
| 26. | Mchana ulikwisha pigwa teke na usiku | Mabadiliko ya kitu, jambo au hali. |
| 27. | Karibu mvi zichukue utawala wote wa kichwa chake | Uzee |
| 28. | Mlima Elgon. Nao pia niliuona kama uliokuwa ukifurahi nami na kunionesha ukarimu. Ulikuwa ukicheka namimi na kunionesha takrima ya Bungoma | Matumaini |
| 29. | Kiza ambacho kilitusindikiza safari yetu usiku wote, kilianza kuikimbia nuru ya alfajiri ili kutoa nafasi kwa weupe wa mapambazuko. | Matumaini mapya |
| 30. | Jinsi mito miwili ile ilivyokumbatiana | Umoja na mshikamano. |

Chanzo: data za utafiti kutoka Mbali na Nyumbani, Julai, 2016.

Jadweli namba 4.3. hapo juu linabainisha tashihisi ambazo zilijitokeza katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Tashihisi hizi zinadhihirisha kuwa msanii ametumia tamathali za usemi kujenga dhamira za kazi yake ya sanaa. Kwa mfano katika mfano namba 13 anasema “Njiani akili yangu ilikuwa ikibishana” hapa msanii kaipa sifa ya kubishana akili, ambapo sifa ya

ubishani ni ya binadamu. Hivyo kwa kutumia tashihisi hii msanii amejenga dhamira ya msongo wa mawazo anaokuwa nao mtu wakati anapokuwa katika hali ya matatizo. Aidha, sambamba na hiyo, mfano namba 27 anasema “Karibu mvi zichukue utawala wote wa kichwa chake” kwa kutumia tashihisi hii msanii anazipa uhai mvi kuwa na uwezo wa kuchukua utawala tendo ambalo linaweza kufanywa na binadamu. Aidha, kwa kutumia tashihisi hii msanii anawasilisha dhana ya uzee ambao tayari mtu anao.

### 4.6.3 Takriri

Ni mtindo wa usemi ambao msemaji hurudia neno au maneno yale yale kwa lengo la kutia mkazo au kusisitiza jambo. Kahigi na Mulokozi (1979) wanaielezea takriri kuwa ni uradidi, yaani urudiaji wa sauti, neno, kirai, kishazi na hata sentensi katika kazi za fasihi. Kwa mfano, katika riwaya ya Mbali na Nyumbani (2013) tunaona msanii ametumia takriri kama vile, “twende! Twende!”, “karibu! Karibu!”.

Katika mifano hiyo, tunaona kuwa msanii ametumia takriri neno ambapo neno moja linarudiwa rudiwa ili kuweka mkazo katika maudhui anayoibua katika kazi yake. Kwa hiyo, takriri hufanya hadhira iweze kutafakari kwa kina suala linalowasilishwa kwa kutumia takriri na hivyo kupata uzito wa maudhui. Mtunzi ametumia takriri kwa lengo la kuipa lugha uwezo wa kubeba fikra au mawazo na ujumbe kuhusu masuala mbali mbali ya kijamii, na kuweka msisitizo wa maudhui. Kwa mfano, msanii anaposema: “Nakufa!Nakufa!”, hapa msanii anasisitiza suala la maumivu makali anayoyapata na kuhitaji msaada

wa wasamaria wema. Katika utafiti huu, ilibainika kuwa msanii wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ametumia takriri katika kuibua dhamira zake. Matokeo haya yanajidhihirisha katika jadweli lifuatalo:

**Jedweli Na. 4.4: Takriri na Uibuaji wa Dhamira katika Riwaya ya *Mbali na Nyumbani***

| Na. | Takriri | Dhamira |
|---|---|---|
| 1. | "Mbona hunijibu, kwani mwanamke hwenda kwa mwanamme kufanya nini?"….. "Hujui ?Hujui?" | Msisitizo |
| 2. | "Kumekucha! Msafiri pwani! Msafiri pwani!" | Utayari |
| 3. | Yakipiga kama vile yalivyokuwa yakipiga mapigo ya moyo wangu uliokuwa umejaa hamu ya safari na kuihimiza treni, ukiiambia, "Twende! Twende!". | Matumaini |
| 4. | "Karibuni! Karibuni!" Shaabani aliwakaribisha. | Ukarimu |
| 5. | "Henya! Henya! Henya! Henya!" Elly aliigeuza hiyo kuwa ndio nyimbo ya kutia hima safari yetu. | Kuhamasisha |
| 6. | "Pesa! Pesa! Kila mtu nalia pesa | Umasikini/Ukata wa pesa |
| 7. | Nilikuwa nikichachatika, nikiomba. "Eeee Mungu, kama mwizi siku zake ni arobaini, mimi bado sikuzitimiza! Nisaidie! Nisaidie!. | Maombi |
| 8. | Nilipiga kelele, "Nakufa! Nakufa!" | Kuhitaji Msaada/Kutaka msaada |
| 9. | "Ndio! Ndio! Nakumbuka kuona jina kama hilo mahali". | Msisitizo |
| 10. | …… alikuja tena na tena na tena, hata hakunidhukuru. | Msisitizo/Mara kadhaa |
| 11. | Kila siku mpya ilikuwa hivyo, labda leo…labda leo. | Huduma mbaya katika sekta za Umma. |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | Yalikuwa yamefungwa marundo marundo | Msisitizo/Kwa wingi |
| 13. | Matiti yalimjaa kifua tele macho yalikuwa yamemregea, akiniita, “Njoo! Njoo!”. | Utayari |
| 14. | Alimpigia kelele, “Daniel! Daniel!” | Msisitizo |
| 15. | Hali ilikuwa ya kiza kiza | Msisitizo |
| 16. | Alikuwa akipiga mayowe. “Mama yangu weee!Mama yangu weeee” | Maumivu |
| 17. | “Kuna njama! Kuna njama! Kuna njama!” umati mkubwa wa watu ulipiga kelele | Ukandamizaji na uonevu |
| 18. | “Pale! Pale! Niliwaonesha wenzangu ile meza tupu. | Umoja na mshikamano. |

Chanzao: Data za utafiti katika Mbali na Nyumbani, Julai, 2016

Jadweli namba 4.4. hapo juu linaonesha baadhi ya takriri alizotumia msanii wa riwaya ya Mbali na Nyumbani. Takriri hizo zinaonesha wazi kuwa tamathali za usemi ni mbinu muhimu inayotumiwa na msanii katika kuibua dhamira zake. Hivyo basi, udhihirikaji huu wa tamathali za usemi unazidi kusisitiza kwamba Shafi Adam Shafi anatumia tamathali za semi kama mbinu ya kuibua dhamira alizozikusudia.

### 4.6.4 Methali

Methali ni semi fupi au kauli ambazo huwa na maana nzito au hekima ndani yake. Kauli hizi huwa zenye busara na mafunzo kuhusu maisha na mahusiano ya watu. Methali hutumia lugha ya mkato ya kuonya au kusisitiza jambo fulani. Ukweli na umuhimu wa methali hutegemea mazingira yanayohusishwa. Aidha methali zinahitaji ujuzi wa kuzifafanua kwa sababu maana zake huwa zimefichwa na mara nyingi huwa ni mafumbo.

Hivyo basi, methali huitajirisha fani na maudhui ya kazi ya fasihi na kutumika kama daraja la kupitishia maadili kwa jamii (Senkoro, 1982 na 2011). Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba methali ni tungo za kimapokeo ambazo hubeba falsafa ya maisha ya jamii husika. Maana ya methali yaweza kukidhi mahitaji ya mtumiaji kwa namna yake kadri ya mazingira na wakati wake lakini bado hekima ya methali hiyo itaendelea kuwa hazina hata kwa mazingira na nyakati nyengine tofauti pia.

Kwa mantiki hiyo, dhima kuu ya methali hujitokeza katika malezi, kwani methali zimejaa maadili ambayo humsaidia mwanadamu na kumwongoza kwenye msingi bora wa maisha. Zinaweza kuwa methali za masuto au za mawaidha. Methali za mawaidha ni zile zenye lengo la kuonya, kuusia, kushauri na kufunza. Methali za masuto huwa na lengo hilo hilo lakini maneno yake ni ya kukaripia na hata kukemea. Kinachobainika kutokana na maelezo hayo ni kuwa dhima kuu ya methali ni kufunza na kulea mtu ili aweze kuoana na matakwa ya jamii yake.

Katika utafiti huu, matokeo yalidhihirisha kuwa mtunzi ametumia tamathali ya usemi ya methali kama mbinu ya utunzi na ujenzi wa dhamira ya kazi yake. Jadweli namba 4.5. linabainisha namna methali zilivyotumika kuibua dhamira za kazi ya fasihi ya riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.

**Jedweli Na. 4.5: Methali na uibuaji wa Dhamira katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani**

| Na. | Methali | Dhamira inayoibuliwa |
|---|---|---|
| 1. | "Ngoma ya kitoto haikeshi" | Mtoto hapangi kitu au jambo likaendelea |
| 2. | "Ukiipata itumie ukiikosa ililie" | Unapopata fursa itumie kwani kuna siku utaikosa wakati unaihitaji |
| 3. | "Penye nia pana njia" | Mafanikio |
| 4. | "Haraka haraka haina Baraka" | Kila jambo linataka ustahamilivu, mafanikio hayapatikani kwa kulazimisha. |
| 5. | "Aumwae na nyoka akiona ung'ongo huogopa" | Tahadhari. |
| 6. | "Jambo usilolijua ni usiku wa kiza" | Ni vigumu kupata picha juu ya jambo usilolifahamu |
| 7. | "Subira huvuta heri" | Mafanikio |
| 8. | Mtaka cha mvunguni sharti ainame | Kujituma |
| 9. | "Leo ni leo asemae kesho mwongo" | Kujali wakati |
| 10. | Mstahamilivu hula mbivu | Anayevumilia shida ategemee mafanikio |
| 11. | "Mwenye macho haambiwi tazama" | Mtu anayeelewa juu ya jambo fulani hapewi maelekezo juu ya jambo hilo. |
| 12. | "Msafiri ni aliye pwani" | Anayehitaji jambo ni yule anayelifuatilia jambo hilo |
| 13. | "Hakuna marefu yasiyo na ncha" | Shida na matatizo mwishowe humalizika |
| 14. | Mwenda tenzi na omo hurejea ngamani | Mtu aende aendako lakini mwishowe atarudi nyumbani |
| 15. | Fimbo ya mbali haiui nyoka | Mtu wako asiyekuwepo hawezi kukufaa/kukusaidia pale unapopatwa na tatizo la ghafla. |

| | | |
|---|---|---|
| 16. | Pokea hidaya ingawa dhaifu | Ushukuru kwa ulichonacho |
| 17. | Baada ya dhiki faraja | Mafanikio hupatikana baada ya kuhangaika. |
| 18. | Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. | Asiyesikia nasaha na maelekezo kutoka kwa wazazi wake, ataishi maisha ya shida duniani. |

Chanzo: Data za utafiti kutoka Mbali na Nyumbani, Julai, 2016.

Jadweli namba 4.5. linabainisha methali na namna zinavyoibua dhamira. Ingawa methali alizotumia msanii katika riwaya hii ni chache lakini zimebeba maudhui mazito ambayo kwa kiasi kikubwa yamejikita katika hali ya kuelimisha na kuadilisha. Kwa mfano, methali namba 7 msanii anaonesha umuhimu wa kuwa na subira, kwani anayesubiri hajuti na badala yake atajikuta akiwa na mafanikio.

### 4.6.5 Tanakali Sauti

Tanakali sauti ni maneno ambayo yanaigiza sauti ya kitu fulani au tendo fulani. Maneno haya yanasaidia sana kuyafanya yale anayoyaeleza mtambaji/mwandishi yaeleweke kwa hadhira yake. Yanasaidia sana kukamilisha hisia za hadhira au msomaji wa habari, kwani mara nyingi hushughulikia milango yote mitano ya fahamu za mtu.

Utafiti huu ulibaini kuwa msani wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ametumia tanakali sauti katika kuwasilisha dhamira za kazi yake. Jadweli lifuatalo linaonesha tamathali ya usemi ya tanakali sauti jinsi ilivyoibua dhamira katika riwaya tuliyoifanyia utafiti.

**Jedweli Na. 4.6: Tanakaulisauti na Uibuaji Dhamira katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani**

| Na. | Tanakali sauti | Dhamira inayoibuliwa |
|---|---|---|
| 1. | Ile ndoto yangu ya kuwa ningelifika Kairo ilikatika, Kap! | Kupoteza matumaini/Kukata tama. |
| 2. | “He! He! He!” alicheka akanitazama | Furaha/ Tabasamu. |
| 3. | Nje majogoo yakiwika. “Kokorikoooo! Kokorikoooo! | Mapambazuko. |
| 4. | Mwendo wa treni ulipamba moto, “Njinga! Njinga! Njinga!” | Mwendo wa kasi. |
| 5. | Roho ilinipiga “Pa! pa! pa!” | Hali ya woga au wasiwasi |
| 6. | Nyenje walipiga kelele, “Nyweee! Nyeee!” | Ishara ya alfajiri |
| 7. | “Shhhhhh!” alimnyamazisha Abdalla | Kuonya/kukataza jambo |
| 8. | “Parrrrr mpaka Makka” | Kuharakisha jambo |
| 9. | Tulikula chakula tukakifuta fyu! | Kukimaliza chote |
| 10. | Moyo ulinipiga “paaaaa”….. | Mshituko |
| 11. | ….na mimi nilitabasamu huku nikipumua. Ofyeeeee!” | Matumaini/Shukurani |
| 12. | Alizifungua chupa moja moja, “tofyo! Tofyo! Tofyo!” mpaka akamaliza kuzifungua zote. | Muendelezo wa tendo |
| 13. | ….injini hiyo ilikuwa ikinipigia kelele, “Kinja! Kinja! Kinja!” | Mwendo wa kasi |
| 14. | Nilitoka pale nilipokuwa nimejificha kwa kunyatia, nyatu! nyatu! | Hali ya kuwa na tahadhari |
| 15. | “Ohoooo! Kima ilikuwa waa, tena nzuri san-naaa”. | Kukubaliana juu ya jambo Fulani |
| 16. | …..Umezama huko ulipokuwepo jii! | Kutorudi tena |
| 17. | Tulipotoka jua lilikuwa tayari limeshajimwaga, mwaaa! | Lishachanganya |
| 18. | ….Niliusikia ukulele ukilalamika, “Yaaa-A-Uaaaa!” | Huzuni |

| | | |
|---|---|---|
| 19. | “Ha! Ha! Ha! Ha!” alicheka | Furaha |
| 20. | “M-m-m-m!” aliguna akatikisa kichwa | Kukubali jambo |
| 21. | Simu yangu ya mkononi ililia, “chirr chirr!” | Wito |

Chanzo: Data za utafiti kutoka Mbali na Nyumbani, Julai, 2016.

Jadweli namba 4.6. hapo juu limebainisha tamathali ya usemi ya tanakali sauti zilizomo katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ambazo zinadokeza dhamira mbali mbali. Kwa mujibu wa utafiti huu, imebainika kuwa riwaya ya Mbali na Nyumbani imesheheni matumizi ya tamathali za usemi ambazo ndizo zinazoibua dhamira za msanii. Imebainika kuwa asilimia kubwa ya dhamira za msanii zimeibuliwa kwa kutumia tamathali ya tashibiha miongoni mwa tamathali za usemi tulizozifanyia utafiti, ikifuatiwa na tashihisi na kwa kiasi kidogo tanakali sauti. Aidha riwaya hiyo imepata nguvu zaidi na kupendeza kutokana na utumiaji mkubwa wa msanii wa tamathali za usemi katika riwaya yake. Jambo hili linadhihirisha kwamba, Shafi Adam Shafi, mtunzi wa riwaya hii anatumia tamathali za usemi kufikisha dhamira zake ikiwa ni kibainishi chake cha mtindo katika utanzu wa riwaya.

## 4.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulika na data zilizokusanywa kupitia kazi teule. Data zimepangwa kutegemea madhumuni mahususi ya utafiti. Uchambuzi wa data ulipangwa kutegemea mpangilio wa maswali ya utafiti huu. Kwa ujumla sura hii ilijibu maswali mawili ya msingi ambayo yaliibuliwa katika sura ya kwanza kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti huu. Sura hii imechambua,

kuonesha na kujadili yafuatayo; kwanza sura imebaini kwamba kuna utumiaji mkubwa wa tamathali za usemi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Pili tamathali za usemi zimetumika kama ni mtindo wa msanii katika kuibua dhamira za kazi yake.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho ambayo imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu muhutasari, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo kwa ajili ya utafiti wa baadae.

## 5.2 Muhutasari

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa tamathali za usemi katika kuibua dhamira katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani.* Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhamira katika tamathali za usemi katika riwaya ya Mbali na Nyumbani iliyotungwa na Shafi Adam Shafi ili kuona jinsi gani vipengele hivyo vinatumika ili kuibua dhamira ya kazi hiyo. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo ni; kwanza, kubainisha tamathali za usemi zilizotumika katika riwaya ya Mbali na Nyumbani, na pili, kubainisha dhamira zinazoibuliwa na tamathali za usemi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani.*

Tatizo la utafiti huu limetokana na uelewa wa mtafiti baada ya kupitia mapitio mbali mbali na kubaini kuwa hakukuwa na utafiti ambao umefanywa wa kuchunguza dhamira katika tamathali za usemi katika riwaya ambayo tumeifanyia utafiti, kwa hiyo, tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza dhamira katika tamathali za usemi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ili kuona ni jinsi gani Shafi Adam Shafi ametumia kipengele hicho katika kuibua dhamira za kazi yake hii. Kwa kufanya hivyo, tumeweza kubaini tamathali za

usemi zilizotumika katika riwaya teule na pia kuibua dhamira katika tamathali za usemi hizo.

Katika sura hii pia, maswali mawili yaliulizwa ambayo ni; je, ni tamathali zipi za semi zinazotumika katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*? Na swali jengine ni je, dhamira zipi zinazoibuliwa kutokana na tamathali za usemi katika riwaya ya Mbali na Nyumbani?

Kwa ujumla maswali haya yalipatiwa majibu katika sura ya nne ambapo zilibainishwa tamathali za usemi zilizochaguliwa kutoka katika riwaya ya Mbali na Nyumbani, lakini pia zilichambuliwa tamathali hizi za usemi ili kuona dhamira zinazoibuliwa katika matumizi ya tamathali za usemi hizo. Halikadhalika, sura hii iliangalia umuhimu wa utafiti ambapo mtafiti aligundua kuwa matokeo ya utafiti huu yatachangia kupata maarifa ya ziada juu ya tamathali za usemi zinavyojenga dhamira katika kazi za fasihi.

Mipaka ya utafiti nayo ilikuwa ni sehemu moja wapo iliyobainishwa katika sura hii, ambapo utafiti huu ulilenga kuchunguza na kuchambua tamathali za usemi katika riwaya moja tu ya Shafi Adam Shafi ya Mbali na Nyumbani, hata hivyo tamathali za usemi zilizochunguzwa ni tano tu ambazo ni tashibiha, tashihisi, takriri,methali na tanakali sauti. Pia katika sura hii tumeeleza vikwazo vya utafiti na utatuzi wake na mwisho ni mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili imefanya mapitio ya kazi tangulizi zinazohusiana na anuani ya utafiti huu. Katika mapitio haya tumeanza kwa kutolea uchambuzi na ufafanuzi wa istilahi

zilizotumika katika utafiti huu, baada ya hapo tumeweza kuzichambua kazi za watu mbali mbali walizozifanya kuhusiana na mada ya utafiti. Wanyonyi (2009) alihakiki riwaya ya Nyuso za Mwanamke ambapo alishughulikia matumizi ya lugha ya kitamathali kama vile tafsida, ishara na uashiriaji na maswali ya balagha.

Watafiti wengine waliofanyia utafiti kuhusiana na tamathali za usemi ni kama vile Too (2011) aliyetafiti tamthiliya ya Nguzo mama (1982) na Penina Muhando, Jilala (2010/2011) katika makala yake ya lugha na ujinsia, Ramadhani (2005)alifanya utafiti wa matumizi ya sitiari katika tamthiliya ya Mashetani ya Ebrahim Hussein na Ngoma ya Ng'wana Malundi ya Emmanuel Mbogo, Mussa (2015) ambaye alichunguza tamathali za usemi katika tamthiliya za Morani na Fumoliongo. Mawazo ya watafiti wote hawa yamechukuliwa na kufanyiwa kazi katika tasnifu hii.

Sura ya tatu, utafiti huu umejadili mbinu za utafiti. Ambapo katika sura hiyo imebainishwa kwamba eneo la utafiti huu ni eneo la Chake chake Pemba hasa katika tawi la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Pemba na Dar es Salaam. Walengwa katika utafiti huu walikuwa ni mtunzi wa riwaya ya Mbali na Nyumbani (2013) Shafi Adam Shafi na wanafunzi wa umahiri wanasoma kozi ya Fasihi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Pemba.
Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi maalum.
Mtafiti aliteua riwaya ya Mbali na Nyumbani ya Shafi Adam Shafi katika utafiti wake huu.

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji machapisho ambayo ilimsaidia mtafiti kuichambua riwaya teule kwa makini na kubainisha tamathali za usemi tulizozifanyia utafiti. Aidha katika uchambuzi wa data za utafiti huu, mbinu ya uchambuzi wa maudhui ilitumika katika kuchambua data za utafiti huu. Utafiti huu umetumia mbinu zisizo za kitakwimu katika kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti.

Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yametokana na maswali mawili ambayo yalitokana na malengo mahsusi. Kwa hiyo matokeo ya utafiti huu ni kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza lililenga kubaini tamathali za usemi tulizozichagua katika riwaya ya Mbali na Nyumbani ambazo ni tashibiha, tashihisi, takriri, tanakali sauti na methali. Ambapo utafiti huu umegundua kuna matumizi makubwa ya tamathali za usemi ya tashibiha ikifuatiwa na tash-hisi kuliko tamathali za usemi nyengine. Hivyo basi, kutokana na utafiti huu umegungdua kwamba Shafi Adam Shafi ni mtumiaji mkubwa wa tamathali za usemi katika uteuzi wa kazi zake za sanaa, hususan ni kazi tuliyoifanyia utafiti.

Swali la pili lililenga kubainisha dhamira zilizoibuliwa na tamathali za usemi katika riwaya ya Mbali na Nyumbani. Utafiti huu umebaini kuwa, tamathali zote zilizotumika katika utafiti huu zimeibua dhamira za msanii. Aidha, utafiti huu unamtaja Shafi Adam Shafi kama ni msanii aliyetumia tamathali za usemi kama ni kipengele muhimu zaidi katika ufanikishaji wa utunzi wa kazi yake hii ya fasihi. Kwa hivyo utafiti huu umebaini kuwa utumiaji wa tamathali za

usemi ni kibainishi cha mtindo wa msanii Shafi Adam Shafi katika utunzi wa kazi yake hii.

Sura ya nne imefanya uwasilishaji wa data na uchambuzi wake. Katika kukamilisha hili, tumechambua na kujadili data zinazoeleza juu ya dhamira zinazoibuliwa na tamathali za usemi katika riwaya ya Mbali na Nyumbani. Sura ya tano ndiyo ya mwisho katika utafiti huu na imewezesha kufanya muhtasari, hitimisho na kutoa mapendekezo ya utafiti wetu kwa watafiti wanaokuja huko baadaye.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kutafiti, kuchunguza na kuchambua data zinazohusiana na tamathali za usemi zinavyoibua dhamira katika riwaya ya Mbali na Nyumbani. Tamathali za usemi katika riwaya hii zilionekana hazijafanyiwa utafiti wa kina. Hali hii ilimpelekea mtafiti kuona ipo haja ya kufanya utafiti huu ili kupunguza pengo hilo la kitaaluma. Utafiti huu unahitimisha kuwa riwaya ya Mbali na Nyumbani imetumia tamathali za usemi kama kibainishi cha mtindo wa msanii Shafi Adam Shafi katika kazi yake hii.

Tamathali hizo huibua dhamira zinazosawiri muktadha wa jamii za Kiafrika. Katika riwaya ya Mbali na Nyumbani mtunzi ameingiza kipengele cha tamathali za usemi ili kusawiri uhalisia wa matokeo ya kijamii.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umechunguza Riwaya ya Mbali na Nyumbani ya Shafi Adam Shafi. Ni ukweli uliodhahiri kwamba, kazi yoyote ile ya utafiti licha ya kuwa

inazungumzia eneo maalum haiwezi kuchambua kila kitu kinachohusiana na eneo hilo. Kwa mantiki hiyo basi, utafiti huu ulichunguza tamathali za usemi katika kuibua dhamira katika riwaya ya Mbali na Nyumbani.

Kwa hiyo kuna vipengele ambavyo havikuchunguzwa kwa sababu havikuwa malengo ya utafiti huu. Hivyo basi, utafiti huu unapendekeza tafiti nyengine zifanyike kwa kulinganisha tamathali za usemi za riwaya ya Mbali na Nyumbani na riwaya nyengine za Shafi Adam Shafi ili kubaini mbinu za kimtindo za msanii huyu zinazobainisha mtindo wake katika utunzi.

# MAREJELEO

Abbas, M.M, (2015). Uchunguzi wa Tamathali za Usemi katika kuibua Dhamira katika Tamthiliya: ulinganishi wa Morani na Fumo Liongo: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (haijachapishwa). Dar es Salaam, Tanzania.

Adam, O. A. (2014) "Kuchunguza Dhima za Kijamii na Kiutamaduni Katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Kuli na Vuta N'Kuvute. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.

Balisdiya, M. L. (1982). Uchunguzi katika Fasihi Simulizi Vizingiti na Mkabala (Makala za Semina). Dar es salaam, TUKI.

Brown, K. na Jim, M. (1991). *2nd Ed Syntax:Alinguistic Introduction to Sentence Structure*, London: Harper Collins Academic Publishers.

Catherine. W. N. (1991). *Misingi ya Nadharia ya Kiswahili.* Nairobi: University of Nairobi.

Chanler, D. (1992). *Semiotics: The Basics,* London: Routledge Press.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika riwaya za Shaaban Robert.* Dar es Salama: TATAKI.

Cooper, R. L. (1989). *Language Planning and Social Change.* Cambridge University Press.

Cresswell, J. W. (2009). *Researcha Design: Qualitative, Quantative and mixed Methods Approaches.* Los Angeles: SAGE Publication.

Diegner, L. (2011). "Mazungumzo na Adam Shafi juu ya Uandishi wake wa Riwaya," Katika, *Swahili Forum 18*(2), 73-68.

Enon, J. C. (1998). “Educational Research, Statistics and Measurement”, Department of Distance Education: Institute of Adult and Continuing Education Makerere University Kampala., Uganda.

Jilala, H. H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

Jilala, H. H. (2010). Lugha na jinsia katika “Ushairi:Uchunguzi wa sitiari za UKIMWI na Mapenzikatika Mashairi ya Bongo Fleva”katika Toleo Maalum la Muziki wa Kizazi Kipya Mulika. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tanzania.

Kahigi, K. K. (1995). “Lugha katika vitabu vya watoto” Kioo cha Lugha, Juzuu na. 1, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Keys, B. (1989). “Four Faces of full Function Middle Manger” *Califonia Management Review, 2(1),* 34 - 46

Kezilahabi, E. (1983). “Utunzi na Riwaya na Hadithi Fupi,” katika, Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili namna 3, Dar es . salaam: TUKI.

Khatibu, M. S. (1983). “Tamathali za Semi za Kiswahili,” Katika Mulika namba 18. Dar es salaam: TUKI.

Kothari, C.R. (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delh: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, R. C. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delh: New Age International (P) Ltd, Publishers.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Masebo, J. A. na Nyangwine, N (2004). *Nadharia ya Fasihi Kidato cha (5) na (6)*. Dar es salaam: Afro Plus Industries Ltd..

Matteru, M. L. (1976). Fani ya Hadithi na Riwaya: Makala katika Kioo cha Lugha. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*, Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mlacha, A. K. S. na Madumulla, J. S. (1991). Riwaya ya Kiswahili. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa fasihi*. Nairobi: East Africa Education Publishers Ltd.

Msokile. B. (1993). *Miongozo ya Lugha na Fasihi. Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press:

Mulokozi, M. M. (1696). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania: Dar es salaam. Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi*: *Katika Mulika 21*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1979). Kunga za Ushairi na Diwani Yetu, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Ndungo, C. M. na Wafula R. M. (1993). *Nadharia ya Fasihi Simulizi (Kiswahili Part III)*. Nairobi: The College of Education & External Studies.

Ndungo, W. C. na Mwai, R. (1991). Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili. Nairobi: Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Ndungo, C. M. na Wafula R. M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. Narocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation

Nkwera, F. M. V. (1979). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Nkwera, F. V. F (2009). Tamrini za Fasihi Simulizi Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: Bussness Printers Ltd.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College: Rock Island.

Owino, J. J. (1978). *Faharasa ya Utafiti wa Amali za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam. TUKI.

Ramadhan, S. K. (2007). Tasnifu ndogo: Uhakiki wa Nafasi ya Mwanamke katika vitabu vya mashairi ya Shaaban Robert na Muhammed Seif Khaitib, Zanzibar SUZA., Zanzibar, Tanzania.

Ruhumbika. G. (2003). “Tafsiri za Fasihi za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili”. Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III (2003). Dar es Salaam, Tanzania.

Said. A. M. (1995). Kunga za Nathari ya Kiswahili. Nairobi: East Africa Education Publishers Ltd.

Saleh, K. K. (2015). Ufasihi Simulizi katika riwaya za Shaaban Robert: Adili na nduguze na Wasifu wa Siti bint Saad: Tasnifu ya Uzamili. (haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Sengo, T. S. Y. (1975). *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi yake*. Nairobi: Foundation Book.

Senkoro, F. E. M. K. (1976). "Utamaduni Katika Riwaya za Kiswahili, Katika Kiswahili, Juzuu namba 46/2, Dar es salaam: TUKI.

Senkoro, F. E. M. K. (1977). "Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Umma," Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria Tanzania, Dar es salaam, Tazania.

Senkoro, F. E. M. K. (1979). *Utamaduni katika riwaya za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es salaam: Press Pulbisity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2012). *Fasihi Andishi*, Dar es Salaam: KAUTTU

Shafi, A. (2013). *Mbali na Nyumbani*. London: Longhorn Publishers.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, (1988). *Kiswahilli Sekondari*. Dar es Salaam: Taasisi ya Ukuzaji Mitaala.

Taib, A. H. (2008). *Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi. Katika Mulika*. Dar es Salaam: TUKI.

TAKILUKI, (1981). *Misingi ya Nadharia ya Kiswahili.* Stockholm: Berlings Arlovs.

TAKILUKI, (1981). *Hapa na Pale.* Zanzibar: TAKILUKI.

TUMI, (1988). *Kiswahili Sekondari*. Dar es Salaam: TUMI.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa* Fasihi. Nairobi: Vide – Muwa.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenex Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications.